SportPesa
TZS. 735,865,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**JWTZ** yaonya utapeli, rushwa uandikishaji kujiunga na jeshi

UKURASA 3




**Neymar kukaa nje wiki nane**

UKURASA 22


# Nipashe

**Jumatano Desemba 1, 2021** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580781

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Marufuku masomo ya ziada likizo na shuleni



- **Waziri** aungana na madaktari, asema yanaathiri afya za watoto...

*Endelea ukurasa 2*



Abiria wakisubiri usafiri katika kituo cha mabasi cha Tegeta Nyuki, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana, ambacho mazingira yake ni mabaya kutokana na kuwa na mashimo makubwa yanayosababisha kujaa maji wakati wa mvua, pia kukosa sehemu za kujikinga na mvua/jua, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa abiria na madereva wa daladala. **PICHA: JOHN BADI**



## Muuguzi, daktari waadhibiwa kwa madai ya mapenzi kazini

UKURASA 3

## Mahakama yatupa pingamizi la Jamhuri kesi ya Mbowe

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA MLIMA MREFU FA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mkurugenzi wa The Guardian Ltd (TGL), Joyce Luhanga, akimweleza jambo Kaimu Balozi wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran nchini, Balozi Hussein Alvand Bahineh (wapili kushoto), alipotembelea kiwanda cha uchapaji wa magazeti ya kampuni hiyo, eneo la Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Uhusiano wa Ubalozi huo, Mohammad Rezaee na kulia ni Meneja Raslimali Watu wa TGL, Emmanuel Matondo. **Picha zaidi Uk. 7.** **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mahakama yatupa pingamizi la Jamhuri kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imetupilia mbali pingamizi la upande wa Jamhuri la kupinga kupokewa nyaraka nne za shahidi wa pili wa utetezi, Lembris Mchome, katika kesi ndogo ndani ya kesi kubwa inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe.

Uamuzi huo umetolewa baada ya hoja za mawakili wa pande zote mbili hivyo kukubaliana na hoja za upande wa utetezi.

Akitoa uamuzi juu ya pingamizi hilo la mawakili wa Jamhuri, Jaji Joachim Tiganga alisema: "Shahidi ana tatizo la kiafya, ni kweli nyaraka zinatumika kuuliza maswali lakini mahakama inayo muda wa kuzichunguza.

"Kwa sababu hiyo mahakama imeona ipokee nyaraka kwa kuzingatia uamuzi wake utakaotolewa mbele, mahakama imepokea barua kielelezo namba 2, 'dispatch', kielelezo namba tatu, hati ya mashtaka kielelezo namba nne na mwenendo wa kesi kielelezo namba 5.

Jamhuri ilipinga kupokewa kwa nyaraka nne za shahidi wa pili wa utetezi katika kesi ndogo kwa madai kuwa vielelezo anavyotaka kutoa havihusiani na shauri lililopo.

Mapingamizi hayo yaliwasilishwa baada ya shahidi kutaka kutoa nyaraka akionyesha alikamatwa na kushtakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kwamba alipokewa na Koplo Msemwa Kituo cha Polisi Oysterbay.

Shahidi alidai alipokamatwa mkoani Kilimanjaro, alipelekwa Kituo cha Polisi Oysterbay Mei, 2020 na alipokelewa na Koplo Msemwa. Alidai kuwa askari huyo hakuwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam mwaka jana kama anavyodai katika ushahidi wake.

Mchome aliiomba mahakama kupokea hati yake ya mashtaka, mwenendo wa kesi yake, barua na 'dispatch' kama kielelezo lakini upande wa Jamhuri ulipinga kwa kutoa sababu mbalimbali.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, alidai nyaraka anazotaka kutoa shahidi zinahusiana na kesi ya jinai namba 77/2020 Jamhuri dhidi ya Lembrus Mchome na ilikuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Alidai hakuna kwa namna yoyote ile nyaraka hizo zikahusiana na kesi iliyopo mahakamani na kwamba hazihusiani kwa namna yoyote na Koplo Msemwa aliyekuwa shahidi wa tatu wa Jamhuri katika shauri dogo.

"Nyaraka hazionyeshi chochote kama Msemwa alifanya kazi Oysterbay Mei 2020. Hazihusiani na ukamatwaji wa mshtakiwa Mohammed Ling'wenya ambaye ndiye shauri lililopo," alidai.

Alidai barua inayotaka kutolewa inatoka Tanafrica Law na imetiwa saini na Wakili Peter Kibatala imeelekezwa kwa Hakimu Mkazi Kisutu, imenakiliwa kwa Lembrus Mchome na Naibu Msajili.

Wakili Hillar alidai hati ya mashtaka na mwenendo wa kesi inahusiana na kosa la matumizi mabovu ya mtandao na shahidi alikamatwa kwa kupiga picha fulani kwa kiongozi fulani. Wakili Mwandamizi Abdallah Chavula alidai shahidi hakueleza nyaraka hiyo ambayo ni hati ya mashtaka ilitengenezwa kutoka kwenye nyaraka ipi.

Akijibu mapingamizi, Wakili wa Utetezi, Nashon Nkungu alidai anaunga mkono upokewaji wa nyaraka zote nne kwa sababu zimekidhi matakwa ya kisheria na kwamba hati ya mashtaka anayotaka kutoa kama kielelezo inahusika sababu ndiyo iliyotumika kumpokea shahidi Kituo cha Polisi Oysterbay.

Wakili Peter Kibatala aliunga mkono kupokelewa kwa nyaraka hizo akidai zimekidhi vigezo vya msingi na shahidi ameweza kutengeneza msingi wa nyaraka hizo na kueleza alivyokaa na vielelezo hivyo kuanzia alipokabidhiwa.

Kesi ndogo imetokana na mawakili wa utetezi kupinga maelezo ya onyo ya mshtakiwa Ling'wenya kupokewa mahakamani kama kielelezo kwa madai kwamba mshtakiwa aliteswa, alitishwa na kusainishwa makaratasi na anadai hakuwahi kufikishwa Kituo Kikuu cha Polisi kama inavyodaiwa na upande wa Jamhuri bali alifikishwa Polisi TAZARA na Mbweni.

Washtakiwa katika kesi hiyo, mbali na Mbowe na Ling'wenya ni Adamu Kasekwa na Halfani Bwire ambao wanashtakiwa kwa madai ya kula njama kufanya vitendo vya kugaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020.

# Marufuku masomo ya ziada likizo na shuleni

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imepiga marufuku masomo ya ziada shuleni baada ya muda wa kawaida, pia wakati wa likizo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu ametamka.

Hatua hiyo inakuja siku sita tangu Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) kitangaze kuanza utafiti wa athari za kiafya kwa wanafunzi wanaobakizwa shuleni kwa muda wa ziada, sambamba na kulazimishwa kubeba mzigo mkubwa wa vitabu.

"Ninaungana nao MAT ambao wameonyesha changamoto kwa serikali tuifanyie kazi. Ninatamka watoto waende likizo, sisi kama TAMISEMI tumepokea kama changamoto ya elimu kutoka kwa waziri, watoto wetu hawapumziki, tabia ya baadhi ya shule za msingi na sekondari kulazimisha muda wa ziada," alisema jana jijini Dodoma.

Waziri katika mkutano wake na waandishi wa habari, alifafanua: "Mihula ya masomo iheshimiwe, watoto wakitakiwa kufunga shule waende nyumbani, kama kuna hitaji la kufanya masomo ya ziada, kipatikane kibali kutoka katibu wa mkoa ili kufanya hivyo likizo."

Akirejea sera mahususi ya elimu iliyopo sasa, waziri aliainisha kuna jumla ya siku 194 za masomo kwa mwaka, akihimza masomo yote yana miongozo na mitaala ambayo ikitumiwa vizuri inatosheleza mahitaji ya kusoma.

Ikiwa ni sehemu ya maelezo yake kuadhimisha miaka 60 ya uhuru wa nchi, Ummy alionyesha kukerwa na kinachojiri kwenye shule, ikiendana na mikasa ya watoto kudhurika, alifafanua "Mtoto wa miaka 12 ana 'depression' (athari kiafya). Nimepata kesi hii, mtoto anaamshwa saa tisa alfajiri hadi usiku."

"Nilipokuwa kwenye mahafali Bagamoyo, nilieleza twisheni mpaka saa mbili usiku... msukumo mkubwa wa kiuchumi na wa mtoto kufaulu mitihani ya badala darasani, kunafanya mtoto kusoma kwa muda mrefu," alisema Ummy.

Mnamo Januari 2, mwaka huu, Nipashe lilitoa ripoti maalum kuhusu kinachojiri shuleni na kuanika picha kamili yenye mifano namna wanafunzi wanavyolazimishwa kukaa muda wa ziada, ikiwa na mifano baadhi ya shule zinazoendesha madarasa hadi saa nne usiku kwa siku saba za wiki.

Ummy alisema serikali imebaini wazazi nao wanachangia msukumo huo wa kufaulu na kusababisha watoto kusoma kwa saa nyingi mradi afaulu, badala ya kuzama katika hoja ya uelewa, jambo alilosema atalisimamia kikamilifu kulikabili kwa kushirikiana na wakurugenzi mikoani, pia makatibu wakuu wa wizara.

Jumatano wiki iliyopita, MAT ilitangaza kuanza utafiti baada ya kubaini athari wanazozipata wanafunzi kwenye shule za msingi, ambao hukaa zaidi ya saa 12 shuleni, kubeba mabegi mazito hususan katika shule binafsi, ikirejea mfano wa shule kadhaa ikiwamo iliyoko Segerea wilayani Ilala.

Inaelezwa shule kadhaa zimebuni mbinu za kulazimisha kuongeza ufaulu, ikiwamo muda wa masomo wa ziada au wanafunzi hao kulazimishwa kukaa bweni.

Kutokana na hali hiyo, MAT ilisema imepokea malalamiko kutoka kwa wazazi kuhusu hali hiyo, ikiwa na maoni ya kubadilishwa muda wa masomo uliopangwa na serikali, kunaweza kuchangia athari kiafya kwa mwanafunzi.

Rais wa chama hicho, Dk. Shadrack Mwaibambe, akizungumza na Nipashe wiki iliyopita, alieleza namna walivyopokea malalamiko kutoka kwa wazazi na walezi na kuanza uchunguzi kubaini athari za kiafya kwa watoto kwa kuwahoji wazazi na shule husika.

"Watoto kulazimika muda wa ziada, kukaa bweni, kubeba mabegi mazito na kukosa muda wa kupumzika na michezo, chama kina wajibu wa kikatiba kuishauri serikali juu ya mambo ya afya," alisema Dk. Mwaibambe.

"Tunataka kujua ukubwa wa tatizo, ushahidi katika suala hilo na shule zinazofanya hivyo tuwe na mifano, tuzungumze na Waziri wa Elimu na kutoa ushauri wa kiafya juu ya afya za watoto."

"Hakuna shule iliyohuru kujifanyia mambo yake inavyotaka bila kujali taratibu zilizowekwa. Shule imekuwa vita kwa watoto wetu. Fikiria mtoto anatakiwa darasani saa 11 alfajiri hadi jioni, darasani hadi saa mbili usiku, ratiba hii ni mpaka Jumamosi, mwaka mzima.

"Mtoto hana ratiba ya kucheza, kukaa na ndugu zake, wazazi wake, anarudi nyumbani amechoka, saa 10 alfajiri ameamshwa. MAT ina wajibu wa kikatiba kuishauri serikali kushughulikia mambo ya kiafya," alisema.

## HABARI KITAIFA




Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, akikata utepe kuzindua kitabu kipya kinachoitwa Misingi ya Ukaguzi katika Sekta ya Umma kilichoandikwa na CAG mstaafu, Ludovick Utouh (kulia) jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Uongozi, Balozi Ombeni Sefue. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JWTZ yaonya utapeli, rushwa usajili jeshini

**Na Beatrice Shayo**

JESHI la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), limeonya vitendo vya utapeli na rushwa vinavyofanywa na baadhi ya watu kuwarubuni vijana wanaotaka kujiunga na jeshi hilo kwa kufanyiwa usajili kwenye nyumba za wageni na kukimbiwa bila kujua.

Kaimu Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano wa JWTZ, Luteni Kanali Gaudentius Ilonda, alibainisha hayo na kutoa onyo wakati akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari kuhusiana na vijana wanaoandikishwa kujiunga na jeshi.

Alisema amelazimika kuzungumza na vyombo vya habari ili umma upate taarifa kwa kuwa kumeibuka tabia, mwenendo na vitendo vya baadhi ya watu ambao wameanza kutumia fursa ya uandikishwaji wa vijana kujinufaisha.

"Wameanza vitendo vya rushwa, vitendo vya kuwalaghai wananchi kwamba watoe fedha ili vijana wao wapatiwe nafasi za kujiunga na jeshi. Huu udanganyifu unaoendelea kufanyika umesababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi, wazazi na ndugu na jamaa ambao wana vijana wao katika kambi za Jeshi la Kujenga Taifa," alisema.

Kanali Ilonda alisema matapeli hao wamefikia hatua ya kuanza kuwasingizia viongozi na makamanda wa jeshi kuwa wametumwa kukusanya hela ili kuwaandikisha hao vijana jambo ambalo si la kweli.

"Mbaya zaidi wamekwenda mbali na wengine kueleza kuwa fedha hizo wametumwa na Mkuu wa Majeshi jambo ambalo si sahihi. Madai kwamba Mkuu wa Majeshi kwa nafasi yake kutuma kuchukua hela aingizwe kijana ni jambo ambalo kwa kweli hatuwezi kulifumbia macho kuona viongozi wetu wanachafuliwa na watu ambao ni wadanganyifu," alisema.

"Jambo la ajabu wanachukua hadi nyumba za kulala wageni wanakusanya vijana, wanawaandikisha majina kwamba subirini tunaenda kuwaletea nafasi za kujiunga na jeshi. Vijana wanakaa pale wanadanganyika na wazazi huyo tapeli kashatokomea. Matokeo yake wanaamua kuja jeshini kumtafuta Mkuu wa Majeshi, makamanda na viongozi wengine kudai nafasi zao," aliongeza.

Kutokana na kadhia hiyo, Kanali Ilonda aliwaomba wananchi kuwapuuza matapeli hao na kamwe wasikubali kudanganyika kutoa fedha kwa sababu ya kuingia jeshini na kwamba hakuna nafasi ya mtu kuingizwa jeshini kwa kutumia mgongo wa fedha, hivyo wananchi wanatakiwa kulitambua hilo.

Pia alisema baadhi ya wananchi wana tabia ya kuwafuata viongozi hasa walioko jeshini, makamanda wa ngazi mbalimbali kwa kuwaomba kuwa vijana wao wako nyumbani na wanaomba waingizwe jeshini.

"Naomba nitumie fursa hii kuwafahamisha kuwa JWTZ lina taratibu zake zilizoainishwa kisheria, kikanuni na lina miongozo ya kuchukua vijana na kujiunga JWTZ. Kamwe jeshi haliandikishi vijana kwa kufuata kigezo cha fedha na haliwezi kufuata mkumbo huo kwani jeshi letu lina uweledi, linafuata maadili, taratibu, kanuni na wana maadili ya hali ya juu," alisema.

SIFA ZA KUJIUNGA

Ili kijana ajiunge na jeshi. Alisema lazima awe ni rai wa Tanzania wa kuzaliwa, awe na umri kati ya miaka 18 hadi 28 na, kijana lazima awe na afya njema ya mwili na awe na afya ya utimamu wa akili. Pia awe mwenye tabia njema na nidhamu, awe hajawahi kupatikana na hatia yoyote ya makosa ya kijinai au kufungwa jela, awe na cheti halisi cha kuzaliwa, vyeti vya shule na vyeti vya chuo kwa wale ambao wamemaliza elimu hiyo.

Kwa upande wa madaktari ambao wameandikishwa, alisema awe amemaliza mafunzo kwa vitendo na kutunukiwa vyeti pamoja na kusajiliwa na bodi husika ya madaktari.

# Wauguzi wasimamishwa tuhuma mapenzi wodini

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, Paul Chacha, ameagiza kusimamishwa kazi watumishi wawili wa Kituo cha Afya Kaliua kwa tuhuma za kufanya mapenzi wodini wakiwa zamu usiku.

Akitoa taarifa hiyo juzi alisema amechukua hatua hiyo baada ya watumishi hao kulalamikiwa na wagonjwa juu ya kujihusisha na vitendo hivyo wanapokuwa zamu usiku.

Alisema baada ya kupata malalamiko hayo aliitisha kikao cha dharura cha watumishi wote ili kujua ukweli juu ya watumishi hao ambao ni muuguzi wa kike (mwajiriwa) na mganga aliyeko mafunzoni waliokuwa wakituhumiwa kufanya mapenzi wodini usiku.

Kiongozi huyo alisema baada ya kujiridhisha kuwapo tuhuma hizo, ameamua kuchukua hatua ya awali ya kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi na hatua nyingine za kinidhamu zichukuliwe na mamlaka husika ikiwa watabainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Alibainisha kuwa kitendo hicho ni utovu wa nidhamu, akisisitiza mtumishi yeyote wa umma na hata sekta binafsi anapaswa kujiheshimu na kutekeleza wajibu wake kwa kufuata taratibu na miongozo ya kazi yake.

"Siwezi kufumbia macho tabia za namna hiyo, tutaendelea kuchukua hatua stahiki kwa mtumishi yeyote asiyezingatia maadili ya utumishi katika eneo lake, huyu mmoja ni daktari mwanafunzi, anajifunza nini sasa kama anaweza kufanya mapenzi wodini?" Alihoji.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya aliagiza kusimamishwa kazi mara moja kwa Mganga wa Hospitali ya Wilaya hiyo, Dk. Irene Apina, kwa tuhuma za kukataa kumpatia matibabu mtoto wa miaka tano na kusababisha kifo chake.

Alisema kitendo cha mtumishi huyo kushindwa kutotoa huduma kwa mtoto huyo kutokana na wazazi wake kukosa fedha za matibabu sio cha kiungwana kwa kuwa alipaswa kutoa huduma kwanza ili kuokoa maisha yake.

Baada ya kupata taarifa za mganga kukataa kutoa huduma kwa mgonjwa (mtoto wa miaka mitano) kutokana na kukosa fedha na kusababisha kifo chake, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Burian, ameagiza akamatwe na kuwekwa ndani wakati akisuburi hatua zaidi za kinidhamu.

Mkuu wa Wilaya huyo pia aliagizwa kumsimamisha kazi muuguzi wa Kituo cha Afya Kaliua, Elias Bwire, kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya utoaji mimba na muuguzi mwenzake Austina Justin kwa kukiuka maadili ya kazi yake.

Akifafanua juu ya tuhuma hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jerry Mwaga, alithibitisha kupokea tuhuma hizo na kubainisha kuwa watazifanyia uchunguzi wa kina na hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya yeyote atakayethitibika kuhusika.

Hata hivyo, alibainisha kuwa mtumishi aliyekuwa mafunzoni hayupo tena katika kituo tajwa, huku akibainisha kuwa hakuwa mafunzoni bali aliletwa na shirika (jina tunalo) ambao ni wadau wa afya kwa ajili ya kusaidia kutoa huduma za utabibu.




HABARI KITAIFA

# Shahidi: Nilifurahi Sabaya kutumbuliwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MFANYABIASHARA Francis Mroso, amedai Mahakamani kwamba alifurahishwa na kitendo cha Rais Samia Suluhu Hassan kumsimamisha kazi na kumtumbua aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Mroso, ambaye ni shahidi wa 10 wa Jamhuri katika kesi ya rushwa na uhujumu uchumi inayomkabili Sabaya na wenzake sita, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Sylvester Nyegu, Enock Togolani, Watson Mwahomange, John Odemba, Jackson Macha na Nathan Msuya.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Fridolin Bwemelo, Mrosso ambaye ni shahidi wa 10 katika kesi hiyo, alidai kwamba kitendo cha Rais Samia kumsimamisha kazi Sabaya kwa ajili ya kupisha uchunguzi kilimfurahisha sana.

Alidai kwamba tukio la Sabaya na wasaidizi wake kulazimisha kupatiwa Sh. milioni 90 lilifanyika Januari 22, mwaka huu.

Pia alidai kuwa alitoa taarifa kwa aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salumu Hamduni, ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alidai kuwa Hamduni naye aliahidi kulishughulikia suala hilo na alimwagiza Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Arusha (RCO), kuchukua maelezo ya tukio hilo na kulifanyia uchunguzi.

Wakili Bwemelo alimuuliza shahidi kwa nini alienda kwa viongozi hao badala ya kwenda Kituo Kikuu cha Polisi na kujibu kwamba Sabaya alikuwa Mkuu wa Wilaya na ni mteule wa Rais, hivyo alikwenda kwa viongozi wa juu zaidi ili walishughulikie tatizo lake la kuchukuliwa kwa nguvu.

Mrosso alidai kuwa alipokuwa Benki ya CRDB Tawi la kwa Mrombo, Arusha, alikuwa chini ya ulinzi na vijana wa Sabaya ambao walijitambulisha kuwa ni maofisa usalama wa taifa na wengine maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hivyo hakutakiwa kupiga simu wala kuongea na mtu yeyote.

Wakili Bwemelo alimwuliza Mrosso kama anamfahamu Cathbert Swai, mfanyabiashara maarufu wa mjini Moshi na kukaa naye kikao chochote, na kudai kuwa hamjui wala hajawahi kukaa naye sehemu yoyote kuzungumzia kitu chochote.

Pia alidai kuwa Kihongosi na Hamduni, hawajui zaidi ya kuwaona na kuwasikia katika shughuli zao za kila siku za kiserikali.

Alidai kwamba alikabidhi Sh. milioni 90 kwa vijana wa Sabaya, wakiwa katika eneo la Shule ya Msingi Sombetini, jijini Arusha, baada ya kuzitoa fedha benki na kuwekwa katika boksi.

Mrosso alidai baada ya kutoka benki aliongozana na vijana hao, hadi katika shule hiyo na aliamuriwa kupunguza mwendo wa gari lake na aliposhuka, kulikuwapo na gari lingine lililokuwa likiwafuata nyuma.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi kifungu cha 57(1) na 60(2) na linawakabili washtakiwa wote.

Ilidaiwa Mahakamani huko, kwamba kwa pamoja washtakiwa hao, Januari 22, mwaka huu, katika maeneo tofauti jijini Arusha, akiwa mtumishi wa serikali kwa nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, walifanya vitendo vya uhalifu kwa kujipatia Sh. milioni 90 kwa manufaa yao.

Shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili Sabaya kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) Sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Ilidaiwa kwamba Januari 22, mwaka huu, eneo la kwa Murombo jijini Arusha, Sabaya alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kumtaka Mroso, kumpatia Sh. milioni 90 kwa kumshinikiza ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo za madai ya ukwepaji kodi. Shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa, linalomkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake, kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Katika shtaka hilo, inadaiwa kwamba Januari 22, Sabaya akiwa katika eneo la Kwa Mrombo, alijihusisha na rushwa kwa kujipatia Sh. milioni 90 kutoka kwa Mroso ili asitoe taarifa za jinai za madai ya ukwepaji kodi.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, inadaiwa kuwa Januari 22, Sabaya akiwa katika eneo la kwa Mrombo, alitumia vibaya nafasi yake ya Mkuu wa Wilaya ya Hai kwa kumtisha Mrosso kumfungulia mashtaka ya kukwepa kodi kitendo ambacho ni kinyume na kifungu cha 15(9) cha Sheria ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa dhumuni la kujipatia fedha.



Mkuu wa Mauzo na Huduma kwa Wafanyakazi wa Mashirika Binafsi na Umma wa Benki ya Absa Tanzania, John Maganga (kushoto), akikabidhi tuzo ya Kampuni Bora ya utengenezaji wa sabuni kwa Mkuu wa Biashara wa Azania Group, Joel Laiser, wakati wa utoaji Tuzo za Chaguo la Mtumiaji Afrika 2021, Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mwanasheria wa Azania, Mahdi Mvungi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jela miaka 40 kusafirisha dawa za kulevya

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara imewahukumu watu wawili kati ya watatu kifungo cha miaka 40 jela na kulipa faini ya Sh. 1,517,853,318 baada ya kupatikana na hatia ya kusafirisha dawa za kulevya.

Hukumu iliyotolewa na Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es salaam aliyeteuliwa kusikiliza kesi hiyo, Jaji Issaya Halfani, baada ya kuridhishwa pasio shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri.

Waliohukumiwa ni Ahmadi Nyamvi na Athumani Mohamedi wakazi wa Wilaya ya Kindondoni mkoani Dar es Salaam, huku ikimwachia huru mshtakiwa wa tatu, Monicar Mathias Murumba, baada ya kutoonekana na hatia.

Baada ya kutiwa hatiani, wakili aliyekuwa anawatetea, Hadson Ndusiao, aliiomba mahakama kuwapa wateja wake adhabu nafuu kwa alichodai ni wakosaji wa mara ya kwanza, pia wamekaa mahabusu kwa muda mrefu, hivyo wanajutia makosa waliyoyafanya na watakuwa raia wema warudipo uraiani.

Jaji Halfani akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 04/2012, alisema kosa la kwanza la kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin aliwahukumu kila mmoja kifungo cha miaka 20 jela pamoja na kulipa faini ya Sh. 1,490,780,580.

Kosa la pili la kusafirisha dawa ya kulevya aina ya cocane aliwahukumu kutumikia kifungo kama hicho jela na kulipa faini ya Sh. 13,535,869 kila mmoja na kufanya ya faini ya Sh. 1,517,853,318.

Jaji Halfani alisema adhabu zote zinakwenda kwa pamoja, hivyo watalazimika kutumikia kifungo cha miaka 20 jela kila mmoja, huku ikimwachia huru mshtakiwa wa tatu Monica Mathias Mulumba.

Awali ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Godfey Mramba, kuwa washtakiwa walikamatwa Januari 11, 2012 katika Kijiji cha Mchinga, Wilaya na Mkoa wa Lindi, wakiwa wanasafirisha dawa hizo zikiwa kwenye madumu na thamani ya zaidi ya Sh. bilioni

# Serikali yaona jambo kitabu cha CAG Utouh

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema kitabu kipya cha masuala ya ukaguzi kilichoandikwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, ni silaha katika kukabiliana na ufujaji wa fedha za umma.

Kitabu hicho kilichopewa jina la 'Principles of Public Sector Auditing - The Case of SAI Tanzania', kilizinduliwa rasmi juzi jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, katika hotuba yake ya uzinduzi wa kitabu hicho iliyowasilishwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Emmanuel Tutuba, alisema kitabu hicho ni silaha muhimu kwa serikali kupambana na wabadhirifu wa fedha za umma.

"Tunakichukua kitabu hiki kama silaha na nyenzo muhimu ya kutuonyesha udhaifu na mapengo ya ukaguzi na kuyafanyia kazi. Kupitia kitabu hiki tutaokoa fedha za umma na rasilimali za nchi," alisema.

Katibu Mkuu alisema ni muhimu maofisa masuhuli na wakaguzi wa ndani wote nchini kununua na kukisoma kitabu hicho kwa kuwa kimesheheni mambo ya msingi kuhusu ukaguzi wa fedha za umma na masuala ya ukaguzi wa hesabu kwa ujumla.

Huku akitoa agizo kwa maofisa wote wanaohusika, kuwa na nakala ya kitabu hicho, alisema kwa kukisoma wataongeza uzoefu wa namna ya kusimamia fedha za umma ili kuepuka migogoro ya kifedha baina yao na serikali.

Alisema kitabu hicho kimetoka wakati mwafaka kwa kuwa serikali sasa inapeleka fedha nyingi katika halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma.

"Kitabu kimeeleza kwa undani namna ambavyo pesa zinakusanywa na kupelekwa kwenye utekelezaji wa miradi ya umma. Sisi kwenye sekta za umma hatukuwa na kitabu kinachoelezea usimamizi wa fedha za umma, lakini kitabu hiki kimekuja muda mwafaka kwa wasimamizi wa fedha za umma ili waangalie uzoefu uliowekwa na Utoah ambaye ni CAG mstaafu.

"Kwa hiyo kupitia kitabu hiki tunaamini kitakwenda kuwaongezea uelewa maofisa masuhuli wetu katika kutekeleza majukumu yao," alisema.

Hata hivyo, Tutuba alimwomba Utouh na Taasisi ya WAJIBU anayoiongoza, kukitafsiri kitabu hicho kwa lugha ya Kiswahili ili kusaidia kila Mtanzania kukisoma na kukielewa kwa wepesi zaidi.

"Kuna baadhi ya watu hawafahamu vizuri lugha ya Kiingereza, pia kuna madiwani ambao wapo katika halmashauri, nao pia wana nafasi katika kusimamia matumizi ya fedha za umma.

"Kwa hiyo kwa wale ambao lugha haipandi watapata shida kutafsiri baadhi ya misamiati iliyoandikwa katika kitabu hiki, hivyo nikuombe Utouh, kama itakupendeza utusaidie kukitafsri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili," aliwasilisha.

Mwandishi Utouh, ambaye ana sifa zingine za awali kabla ya kuwa CAG, mhadhiri mwandamizi wa uhasibu, pia Mkurugenzi wa Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA), ana maelezo kadhaa yaliyomsukuma kuandika kitabu hicho.

Anafafanua kwamba ameandika kitabu hicho baada ya kubaini kuwapo uelewa mdogo na kukosekana vitabu katika eneo la taaluma yake panapogusa mahususi ukaguzi wa hesabu za fedha kwenye sekta ya umma.

"Hiki kitabu kinazungumzia somo ambalo linafundishwa vyuoni lakini kusema ukweli somo lile halina maandishi yoyote kwa mfumo wa kitabu.

"Kwa hiyo utakuta kwamba somo lile lilikuwa linafundishwa kwa kuzingatia katiba na sheria inasemaje, hata nilipokuwa ninafundisha Chuo Kikuu cha Mzumbe, niliona hiyo shida. Baada ya kuwa CAG, nikaona bado tatizo linaendelea watu kutokuelewa ukaguzi katika sekta za umma.

Akiwasilisha hotuba ya CAG, Charles Kichere, Naibu Mkaguzi Mkuu Ofisi ya CAG, Salina Mkumba, alisema kitabu hicho kimezingatia vigezo vyote vya kimataifa katika ukaguzi.

"Kitabu hiki si tu kwamba ni faida kwa Tanzania, bali pia nchi zingine nje ya mipaka ya nchi yetu ikizingatiwa kuna nchi 26 barani Afrika zinazozungumza lugha ya Kiingereza.

## Mongella: Uongozi umegeuzwa biashara

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWANASIASA mkongwe nchini, Balozi Getruda Mongella, amesema hivi sasa watu wanautazama uongozi kama biashara badala ya kujitolea, kwa lengo la kuwatumikia wananchi.

Alisema hayo wakati akihojiwa kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na runinga ya ITV kuhusu tathmini ya hali ilivyokuwa baada ya Tanganyika kupata uhuru miaka 60 iliyopita na hali ilivyo sasa baada ya uhuru.

"Watu kutoridhika na uchaguzi mbalimbali tulionao ambapo mtu anajiona asipochaguliwa yeye, uchaguzi haujawa halali, badala ya kusema tupeane mikono utajaribu siku nyingine, haya yote ndio yamesababisha uongozi uwe kama biashara," alisema Mongella ambaye alikuwa waziri katika serikali ya awamu ya kwanza na ya pili pamoja na kuwa Rais wa Bunge la Afrika.

Mongella ambaye wakati ule alikuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, alisema hivi sasa mtu ambaye hakuchaguliwa anajenga uadui kwa yule aliyechaguliwa na kuanza kuwauliza watu kwanini hawakumpigia kura badala ya kujiuliza na kufanya tathmini ni kwanini walio wengi hawakumchagua.

Alisema watu lazima wafahamu kuwa kazi ya siasa ni ya kujenga nchi na sio ya kutafuta vyeo na hata kama vyeo hivyo vinapokuwapo vinatafutwa, lakini kisiwe ni kipaumbele cha kwanza na cha muhimu.

Mongella alisema siasa tuliyonayo hivi sasa hadhani kama watu wanaielewa na ndio maana mtu asipochaguliwa yeye anaona kama vile nchi haina kiongozi, badala ya kuelewa kwamba siasa ni kama demokrasia, ambayo ni uhuru wa watu wenyewe kusema wanamchagua mtu fulani.

"Nadhani sasa turudi madarasani angalau kuokoa umma wa Watanzania ambao hawana maarifa juu ya siasa, siasa tuifundishe upya tusione aibu... serikali yetu kuwa na mihutasari au silabasi ambazo zinajenga mtu kuelewa siasa na hili lifanyike katika chama chochote," alisema.

Alipoulizwa kwanini hivi sasa kila anayesaka uongozi lazima atumie fedha kununua wapigakura, alisema hali hiyo inatokana na kutojiamini kwani mtu asiyejiamini lazima atatumia njia mbovu za kununua wapigakura ambao baadhi wanaendekeza njaa.

Akiongeza kuwa baada ya miaka 60 ya uhuru lazima tutafute falsafa ya kujitegemea, mtu aone aibu na kubeza mtu anapompa senti na kusema ngapi hizi, jambo alilosema ni aibu.

Mongella alisema wananchi wafahamu kuwa ukimchagua kiongozi aliyekupa fedha kamwe hawezi kukuletea maendeleo.

"Nitakuwa mjinga kiasi gani nikupe milioni halafu niende nashinda vijijini nafundisha watu kusoma na kuandika, niende vijijini kuona nyumba bora zinajengwa, nikafanye nini wakati hela yangu nimekupa, si tumemalizana," alisema na kuongeza:

"Mimi nilikuwa nawaambia wapigakura unakuja nikupe Sh.200 za kwenda kununua gongo mimi nakwenda kupata mshahara wa miaka mitano wapi na wapi, afadhari unipe kura yako bure ili na mimi nikazane na kujenga nchi." Alisema zamani rushwa inayotembea siku hizi haikuwapo, na kwamba ambapo ilikuwa ukiingia kwenye kugombea unamwomba Mungu wako na unamwomba binadamu akupigie kura basi.

"Nilikuja kujifunza mbinu ya kuomba kura, ukiomba kura usiombe zote, wewe ambaye hutaki kunipa acha, lakini usinivurugie, usiingilie uhuru wangu," alisema.

Akizungumzia kuhusu demokrasia, alisema: "Demokrasia haiji kama mtu hashibi, haiji kama hajui kusoma, demokrasia kwa upana wake kwanza ni uwezo wa mtu kuelewa upo wapi, nafasi yako ni ipi, lakini usivuke mipaka ya wenzio, ukivuka filimbi inapigwa."

# Dodoma, Mwanza kicheko mabasi ya mwendokasi

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, amesema kuwa baada ya usafiri wa mabasi yaendayo kasi - mwendokasi kufanikiwa jijini Dar es Salaam, mkakati unaofuata karibuni ni kupeleka huduma hiyo majiji ya Mwanza na Dodoma.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Dodoma kutoa orodha ya mafanikio ya nchi katika miaka 60 ya Uhuru, alitaja sura mojawapo ya mafanikio ni kuokoa muda wa usafiri kutoka eneo moja hadi lingine kutoka wastani wa saa tatu hadi dakika 45.

Waziri alisema ni hatua iliyoongeza tija na ufanisi kwenye usafiri wa umma, ikiwamo kuongeza uchumi wa watumiaji usafiri huo kutokana na kuwahi kufika waendako.

Alisema pamoja na changamoto zilizopo kwenye usafiri wa umma jijini Dar es Salaam, ikiwamo mrundikano wa abiria katika vyombo vya usafiri wa umma, bado mwendokasi umeleta mabadiliko chanya kwa safari ndani ya jiji.

"Utafiti tumefanya na kubaini kuna ongezeko la watumiaji wa usafiri wa mwendokasi kutoka 76,000 kwa siku tangu mradi kuanzishwa (mwezi Mei mwaka 2016) na kufikia hadi abiria 200,000 mwaka 2018.

"Katika usafiri wa mwendokasi mijini, Tanzania inafanya vizuri kwenye usafiri wa umma, ikilinganishwa na nchi kadhaa kama za Afrika Kusini, Nigeria, Misri. Dar es Salaam ina idadi kubwa ya wasafiri wa umma kwa siku," alisema Waziri Ummy.

Alisema mradi wa mwendokasi jijini umechangia ujenzi wa taswira ya jiji na kupokea tuzo kutoka nchi mbalimbali, pia wageni kufika kujifunza jijini Dar es Salaam, kuhusu uendeshaji usafiri wa umma.

"Mradi huu umewezesha wataalamu wa ndani kubuni mfumo madhubuti wa ukusanyaji mapato. Mwaka 2008 hadi 2009 zilikusanywa Sh. milioni 127.7, na kufika Sh. bilioni 11.2 hadi Agosti mwaka huu," alisema.

Waziri Ummy pia alisema usafiri huo ulioboreshwa kutoka mfumo wa kawaida wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) hadi mwendokasi (UDART), ulitokana na ongezeko la mahitaji ya usafiri wa umma jijini pamoja na kuruhusu wamiliki binafsi kutoa huduma, ingawa dosari haikutatuliwa.




Meneja Mawasiliano wa Afrika wa Kampuni ya Justdigit, Meron Bezabeh (wapili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampeni ya kupanda miti kutunza mazingira na kuondoa ukame. Wengine ni Meneja Programu wa Lead Foundation, Njamasi Chiwanga (kulia), Balozi wa kampeni hiyo, Benard Paul maarufu Ben Pol (wa pili kulia) na Ofisa Mawasiliano Bollore Transport Logistics, Fey Mallonga. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Umeme vijijini wafikia asilimia 70

**Na Halfani Chusi**

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) umebainisha mafanikio tisa yaliyopatikana kwenye eneo lake la kazi wakati nchi ikiadhimisha miaka 60 ya uhuru.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema upatikanaji wa umeme maeneo ya vijijini ulifikia asilimia 69.9 mwaka jana.

Alibainisha kuwa tangu kuanzishwa kwa wakala huo mwaka 2005 na kuanza rasmi kazi zake miaka miwili baadaye, umepata mafanikio mengi ikiwa ni pamoja na kuwezesha ujenzi wa jumla ya kilomita 38,296.56 za umeme wa msongo wa kati, kilomita 35,253.43 za umeme wa msongo mdogo, ufungwaji wa mashineumba (transforma) 13,700 na uunganishaji wa jumla ya wateja 716,847 kwa gharama ya Sh. bilioni 2,661.93.

"Mbali na mafanikio hayo, tumepata mafanikio mengine tisa tangu kuanzishwa kwa wakala ikiwamo kutengeneza masoko kwa viwanda vya ndani vinavyozalisha vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa miradi ya umeme.

"Kufikisha na kusambaza umeme katika makao makuu ya wilaya zote, kufunga mifumo ya umeme katika nyumba za wafanyakazi 831 kwenye sekta za afya na elimu katika mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Kagera, Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Tabora.

"Kuwezesha uboreshwaji wa kilimo cha umwagiliaji katika mashamba likiwamo shamba la Mtakuja - Kilimanjaro, Zuzu-Dodoma, kupunguza uhamiaji wa vijana kutoka vijijini kuja mjini kwa kuwa sasa huduma za umeme zinapatikana hadi vijijini.

"Kuanzishwa kwa viwanda vidogo na vya kati mfano mashine ya kusaga, uchomeleaji, saluni za kiume na kike, viwanda vya useremala.

"Upatikanaji wa burudani vijijini mfano matumizi ya televisheni, redio, disko, ujenzi wa mitambo ya baiogesi 725 katika maeneo mbalimbali vijijini kwa ajili ya kuanzisha nishati ya kupikia na kuimarika kwa ujasiriamali vijijini mfano uanzishaji wa vikosi vya kuuza vinywaji baridi, matumizi ya mitandao M-Pesa, Tigo-Pesa," alibainisha.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alidokeza vikwazo vinavyowakumba wakati wa kukamilisha miradi yao vijijini ikiwa ni pamoja na baadhi ya wananchi kutokuwa tayari kutumia umeme, kuharibiwa kwa miundombinu ya umeme ikiwamo nguzo kwa baadhi ya vijiji, kushindwa kumudu gharama za kusukia waya kwa ajili ya kupokea umeme kwa mkazi, uwapo wa vishoka ambao wamekuwa wakiwalaghai wananchi na kuwapandikizia maneno ya uongo juu ya miradi hiyo.

Kamishna Msaidizi Maendeleo ya Umeme, Styuden Rwebangila, aliitaja mikakati iliyowekwa na REA kuendelea kufikisha umeme sehemu ambazo haujafikiwa ikiwa ni pamoja na kuhamisha na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya nishati na umeme vijijini.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Viwanda viongeze uzalishaji sukari

**KILA** mwezi Machi hadi mwishoni mwa Mei kila mwaka viwanda vya sukari nchini vinapokuwa kwenye matengenezo ambacho ni kipindi cha mvua nyingi, uzalishaji wa sukari husimama kwa muda, hali inayosababisha upungufu wa sukari na wakati mwingine bei kupanda .

Licha ya mikakati ya mara kwa mara kukabili upungufu wa sukari nchini, bado uhaba umekuwapo kiasi cha wananchi wengi kuathirika kwa kushindwa kutumia bidhaa hiyo kwa muda fulani.

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo mwaka huu ilisema katika mwaka 2021/22 Wizara kupitia Bodi ya Sukari itahamasisha uzalishaji wa sukari kufikia tani 450,000 ambayo ni mahitaji ya nchi.

Ili kufikia lengo hilo bodi itafunga mitambo miwili ya maji moto itakayotumika kuzalisha mbegu bora za miwa katika mashamba ya pamoja ya wakulima wadogo yenye ukubwa wa hekta 200 katika wilaya ya Kilombero.

Bodi itahamasisha matumizi ya mbolea na kutoa mafunzo kuhusu mfumo wa ununuzi wa pamoja wa mbolea kwa vyama 28 vya ushirika vya wakulima wa miwa.

Aidha, bodi ilisema itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba mawili ya pamoja yenye ukubwa wa hekta 100 yaliyopo Kilombero, itaanzisha mashamba matatu ya mfano ya miwa katika maeneo yanayolimwa miwa ya Mtibwa, Kagera na Manyara.

Katika kukabiliana na uhaba huo, baadhi ya viwanda vina mkakati wa kuongeza uzalishaji kama ilivyofanya kampuni ya Sukari Kilombero imeongeza mtaji kutoka Sh. bilioni 340 hadi Sh. bilioni 700 kwa mwaka.

Kiwanda hicho kinasema mradi huo wa upanuzi utakaohitaji uwekezaji mpya wa awali wa zaidi ya Sh. bilioni 550, ukijumuisha kiwanda kipya kitakachokuza uwezo wa kampuni hiyo wa kutengeneza sukari na kupunguza uhaba nchini.

Wanasema lengo jingine ni kuhakikisha nchi inaondokana na upungufu wa bidhaa hiyo na nchi kujitosheleza ifikapo 2025, kwa kuwa utaongezeka kutoka tani 126,000 hadi 271,000 kwa mwaka na kuisaidia serikali kuokoa dola za Marekani milioni 70 za kuagiza bidhaa hiyo nje.

Pia, kiasi cha miwa kutoka kwa wakulima mwaka 2026/27 kwa takribani tani milioni moja kwa mwaka zaidi ya tani 600,000, ili kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo na kuboresha miundombinu na huduma za kijamii, ikiwamo kuongezeka kwa ajira 2,000 za kudumu na za mkataba 2,440.

Hii ni habari njema kwa kuwa itasaidia kupunguza uhaba wa sukari, pia tunaamini viwanda vingine vina mkakati kama huu kuhakikisha sukari ya kutosha inapatikana nchini.

Uhaba wa sukari uliibuka tena kwenye mkutano wa Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, ambaye alisema nchi hiyo ilitaka kuingiza sukari nchini, lakini walishindwa kutokana na kauli ya Waziri, ndipo Rais alimwambia suala hilo limekwisha wanaruhusiwa kuleta bidhaa hiyo nchini.

Tunaamini viwanda vikiongeza uzalishaji haba wa sukari utakwisha, lakini hilo litawezekana ikiwa wadau wote watahusika ikiwamo serikali kusikiliza kero za wazalishaji.

Kama viwanda hivi vingeanza uzalishaji mpango ulikuwa mzuri wa kuhakikisha wazalishaji wa nje wanauza miwa yao kwa kiwanda, na walihamasishwa kulima lakini hali haikuwa hivyo.

Kuna umuhimu Bodi ya Sukari ikahamasisha wawekezaji kuwekeza kwenye sekta hiyo ili kuepusha kuagiza kutoka nje na badala yake kuuza kwa nchi jirani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

# Muungwana Lazima Nilonge

## Umoja wa kinamama ngazi ya kufikia 50/50

**KILIO** cha muda mrefu cha wanawake ni kutaka usawa wa kijinsia kwenye nyanja mbalimbali kuanzia kwenye uongozi wa kisiasa na wa kuteuliwa ili idadi yao ilingane na ya wanaume katika uwiano wa 50 kwa 50.

Wanawake kama ambavyo wamekuwa wakijinasibu kuwa idadi yao ni kubwa kuliko wanaume, na ni wapigakura wakuu, ambao wana uwezo wa kumpa ushindi mgombea kutokana na wingi wao.

Pamoja na uwingi huo, bado kumekuwapo na malalamiko kwamba hawashirikiani na pale baadhi yao wanapojitokeza kuwania nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali hawapati ushirikiano wa kutosha.

Kama kuna ugumu huo ni vyema kulimaliza na kulifanyia kazi, kwani kwa wingi wao wakiamua kuungana, ni wazi watawabwaga wanaume katika nafasi za udiwani ,ubunge na hata urais.

Kuendelea kutengana kunaweza kuchelewesha kutimiza ndoto yao ya kutaka usawa wa kujinsia, katika nafasi mbalimbali za uongozi na kuendelea kubaki wasindikizaji wa wagombea wa kiume.

Kinamama wamewahi kulalamika katika matukio mbalimbali kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka jana kwamba baadhi yao walibaguliwa na wanawake wenzao na kukejeliwa kwamba hawafai.

Nadhani njia mojawapo ambayo inaweza kuwasaidia kufikia wanachokihitaji, ni kushirikiana na kuachana na hisia za kiitikadi za vyama, badala yake waangalie sifa na vigezo na kumchagua mwanamke mwenzake ambaye wanaona anafaa.

Kigezo kikiwa ni itikadi ya chama, mfumo huo unaweza kuchukua muda mrefu kufikia uwiano wa 50 kwa 50 katika uongozi, kwani wajanja watatumia udhaifu huo kuendelea kuwabwaga.

Hivyo, wanapopanga kuziba kila njia za ubaguzi wa kijinsia, ni muhimu wazibe kuanzia ndani, kwani bila kufanya hivyo, wanaweza kuendelea kuwa wapigakura na wasindikizaji katika uchaguzi.

Kimsingi wanaume wanaweza kutumia udhaifu huo wa kubaguana, waendelee kushika nafasi nyingi za uongozi, hivyo ni vyema wanawake wakajiongeza, ili kumaliza kasoro ndogondogo zinazokwamisha umoja wao.

Malalamiko ya wanawake kukosa ushirikiano katika uchaguzi yapo, hivyo ingefaa viongozi na jumuiya zao kufuatilia kwa lengo la kumaliza kasoro hiyo, ili utengano kuondoka miongoni mwao na kuwafanya kuwa kitu kimoja.

Kwa ujumla, wanawake wanaweza kuwa chachu ya kuziba pengo la usawa wa kijinsia kwa kuachana na ubaguzi miongoni mwao, ili anapojitokeza mmojawapo kuwania uongozi, basi wamchague bila kujali chama anachotoka.

Kutokuwapo kwa usawa wa kijinsia na ubaguzi kwa wanawake na wasichana kunatajwa kama ukatili ambao unapaswa kushughulikiwa na wanawake wenyewe ndani na hata nje.

Ushirikishwaji wa wanawake katika nafasi mbalimbali ni jambo muhimu kwa ajili ya kupanga na kuleta maendeleo na kusaidia kuzuia migogoro inayokwamisha maendeleo jumuishi.

Katika karne ya 21 vuguvugu la haki za wanawake limeshika kasi na kuwafanya baadhi ya kinamama kushika nyadhifa mbalimbali serikalini na hata katika mashirika na kampuni ingawa bado kuna haja ya kasi hiyo kuwa kubwa.

Ninaamini kwamba njia ya kumaliza tatizo inategemea jinsi wenyewe wanavyoimarisha umoja na kuacha kubaguana kwa itikadi za vyama kama, ambavyo imekuwa ikitokea, kwa baadhi yao.

Wasiposhirikiana wanaweka utengano, ambao unasababisha udhaifu, wanapotafuta usawa wa kijinsia, kwani wanashindwa kwa kukosa umoja.

Usawa wa kijinsia ni suala la utawala hasa kutokana na ukweli kwamba dunia imetawaliwa na mfumo dume yenye utamaduni unaoongozwa na wanaume na imekuwa hivyo kwa karne nyingi.

Mfumo huo ulianzishwa kuhusu urithi kupitia wanaume na hadi sasa unaendelea kuathiri kila nyanja ya maisha na unachangia kudumaza maendeleo.

## HABARI PICHA

# KAIMU BALOZI WA JAMHURI YA IRAN, BALOZI HUSSEIN ALVAND BAHINEH ATEMBELEA THE GUARDIAN LTD.




Balozi Hussein Alvand Bahineh akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Kampuni ya The Guardian Ltd. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**



Balozi Hussein Alvand Bahineh (kushoto), akitoa zawadi kwa Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga baada ya kutembelea kampuni hiyo.



Meneja wa Kiwanda cha Uchapaji cha The Guardian Ltd, Balasubramaniyan Venkadachalam (kulia), akionyesha kwa Balozi Hussein Alvand Bahineh, jinsi magazeti yanavyochapishwa.



Kaimu Mhariri wa Gazeti la Nipashe, Epson Luhwago, akimtambulisha Kaimu Balozi wa Jamhuri ya Iran hapa nchini, Balozi Hussein Alvand Bahineh (kushoto), alipotembelea chumba cha habari cha magazeti ya The Guardian Ltd (TGL), mkoani Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga.



Balozi Hussein Alvand Bahineh (wapili kushoto), akizungumza na uongozi wa kampuni ya The Guardian Ltd jana.

# Chuo cha Ardhi Morogoro chapewa mikakati kukamilisha urasimishaji

**Na Munir Shemweta,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekitaka Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) kujipanga na kumaliza urasimishaji makazi katika maeneo kiliyopewa kazi hiyo.

Hatua hiyo inatokana na Dk. Mabula kuelezwa na Mkuu wa Chuo, Huruma Lugalla, kuwa moja ya changamoto kubwa katika urasimishaji makazi maeneo mbalimbali ambayo chuo hicho kimechukua kazi hiyo ni kasi ndogo ya uchangiaji gharama kutoka kwa wananchi.

"Mheshimiwa Naibu Waziri uchangiaji katika urasimishaji makazi katika maeneo mbalimbali nchini tunayoyafanyia kazi hasa hapa Morogoro ni mdogo sana licha ya gharama kupungua kutoka Sh. 150,000 hadi 130,000," alisema Lugala.

Pamoja na kuelezwa changamoto hiyo, Dk. Mabula ambaye alikuwa akizungumza na uongozi wa chuo hicho, juzi alikitaka kuhakikisha kinachukua maeneo machache ya kuyafanyia kazi badala ya mengi ambayo yanaweza kuwashinda kukamilisha kazi kwa wakati.

" Ni vizuri mkajipanga katika urasimishaji. Baada ya kufanyika kosa la awali sasa msirudie tena kosa maana haitaleta picha nzuri kwa chuo. Mnachotakiwa ni kujipanga na kuwa na mkakati wa kukamilisha kazi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, alishangazwa na maelezo kuwa baadhi ya wananchi katika mkoa wake wamekuwa wazito kuchangia gharama za urasimishaji makazi holela wakati wanaweza kujenga nyumba ya Sh. milioni 20 huku wakishindwa kuchangia Sh. 130,000.

"Yaani wananchi wanashindwa kuchangia gharama za urasimishaji wakati wanajenga nyumba kwa gharama kubwa kama Sh. milioni 10 mpaka 20? Hii haina afya kabisa," alisema Shigela.

Awali, Lugalla alimweleza Naibu Waziri kuwa chuo chake kinaendelea na utekelezaji miradi ya urasimishaji makazi katika mitaa 61 nchini kwa kushirikiana na halmashauri na wananchi wanaomiliki ardhi ya makazi yaliyoendelezwa holela.

Kwa mujibu wa Lugalla, jumla ya viwanja 30,188 vimeidhinishwa kufanyiwa kazi ya urasimishaji makazi, viwanja 129, 761 vimetambuliwa huku michoro 218 ikisanifiwa na takriban Sh. bilioni 2.553 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Aidha, mkuu huyo wa chuo aliwasilisha ombi la kutaka kusaidiwa uendelezaji eneo la ekari 33 lililoko Mlima Kola, Manispaa ya Morogoro, kwa ajili ya kupanua wigo wa mafunzo, miundombinu sambamba na kuongeza udahili wa wanafunzi.

Kutokana na ombi hilo, Shigela alisema ni vyema taasisi za umma zinapoomba msaada wa uendelezaji maeneo, zikafikiriwa kusaidiwa na kuongeza kuwa mkoa wake uko tayari kusaidia pale utakapoona mipango ya chuo kuhusu uendelezaji eneo hilo.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus (kulia), akikabidhi kadi ya pikipiki ya magurudumu matatu kwa mshindi wa Shindano la Bonge la Mpango inayoendeshwa na benki hiyo, kwa Derick Jasson Kazindaki kwenye hafla fupi iliyofanyika viwanja vya Stendi ya Buzuruga, jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hisa za NICOL zapaa soko la hisa

**Na Joseph Mwendapole**

HISA za Kampuni ya NICOL Investment PLC, zimeendelea kupaa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kutoka Sh. 170 hadi Sh. 250.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Erasto Ngamilaga, alisema hayo jana alipokuwa akitangaza mkutano mkuu wa mwaka wa wanahisa unaotarajiwa kufanyika keshokutwa.

Alisema wanahisa wa kampuni hiyo wanatarajia kukutana kujadiliana kuhusu maendeleo ya kampuni yao kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam. Alisema moja ya ajenda ni kujadili mafanikio ambayo kampuni imeyapata tangu iliposajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na kwamba mkutano huo ni wa kila mwaka.

"Tunawakaribisha wanahisa wote waje watoe michango mbalimbali waone kampuni yao inaendeleaje kwani tunaendelea kupata mafanikio makubwa sana. Sasa tumeanza kutawanya uwekezaji wetu na tayari tumewekeza Sh. bilioni 14 kwenye hati fungani," alisema

Alisema NICOL imeendelea kuimarisha uwekezaji wake kwa upande wa hisa na tayari imewekeza kwenye mashirika mbalimbali kupitia DSE zaidi ya Sh. bilioni 80. Alisema hayo ni mafanikio makubwa ambayo yamechangia ongezeko la faida la zaidi ya asilimia 43 ambalo limetokana na kuongezeka kwa mapato kutoka kwenye gawio.

Ofisa mtendaji mkuu huyo alisema kulinganisha na miaka iliyopita, NICOL imeendelea kufanya vizuri mwaka 2020/21 na mwaka huo ilitangaza faida ya Sh. bilioni 3.8 kutokana na jitihada za menejiment kutawanya uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali yenye faida.

Ngamilaga alisema kutokana na mafanikio hayo, bodi ya kampuni hiyo kwenye kikao cha Ijumaa itatoa mapendekezo ya gawio kwa wanahisa wake na yakiridhiwa malipo hayo yatafanyika mwaka huu.

"Tunaomba wanahisa washiriki mkutano huu kwa nia ya kuona maboresho yanayofanyika kwenye kampuni yao na kampuni yao inavyozidi kusonga mbele kwenye soko la hisa na namna hisa zao zinavyozidi kupanda thamani kwa asilimia 40 kutoka Sh. 170 mpaka sh 250," alisema.

"Ni matumaini yetu kwamba katika jitihada ambazo tunazifanya na mipango ambayo tumejiwekea NICOL inapanga kupaisha thamani ya hisa zetu hadi hisa moja kuuzwa kwa Sh. 1,400 ambayo ndiyo thamani halisi ya uwekezaji wa NICO kwa uwekezaji wetu," aliongeza.

Alisema kaulimbiu yao mwaka huu ni kuongeza mapato ya kampuni hiyo ili watu wengine wavutiwe kuwekeza na NICOL imechangia kodi mbalimbali serikalini na mwaka huu pekee, imelipa Sh. milioni 300 kama kodi.

## Wabuni mbinu mpya za kuozesha watoto

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Mwakata, Msalala mkoani Shinyanga, wamebuni mbinu mpya ya kuwaozesha watoto wa kike ambao wana umri wa kwenda shuleni kwa kusingizia wanawapeleka kwa shangazi zao walioko mikoani kuendelea na masomo jambo ambalo si kweli.

Pia kata hiyo imetajwa kuongoza kwa ukatili wa kijinsia ulioкithiri wa kutupa watoto wadogo, ubakaji kwa wanafunzi na wazazi kukimbilia kutafuta maisha kwenye migodi ya wachimbaji na kusababisha watoto kukosa mahitaji na wengine kuacha masomo.

Mwenyekiti wa kijiji cha Magunhumwa, Salum Mohamed, alisema hayo wakati wa mafunzo ya rufani kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia, watoto na wanawake chini ya mradi wa kupunguza athari za maafa (KAMA) unaotekelezwa na Shirika la Huheso Foundation kwa kushirikiana na Rudi kwa ufadhili wa OXFAM Ubelgiji.

Alisema baadhi ya wazazi bado wanaendelea kufanya vitendo vya kikatili kwa watoto wa kike kwa kuwanyima haki zao ikiwamo elimu na badala yake wamebuni mbinu mpya ya kuwaozesha kwa kusingizia wanawapeleka kwa shangazi zao.

"Hivi karibuni binti wa miaka 16 alitumwa dukani na wazazi wake wakati anarejea alibakwa na mtu ambaye mpaka sasa hatujamfahamu. Tulimpeleka mtoto hospitalini akawa chini ya uangalizi maalumu lakini mwisho wa siku baada ya vipimo alibainika kuwa na maambukizi mapya ya VVU," alisema Mohamed.

Naye Stella Michael alisema vitendo vya kikatili ndani ya familia muda mwingine vimekuwa vikitokea wakati kinababa wanapotumia dawa aina ya mihadarati na pombe kali ambayo wanapofika majumbani wanaanza kupiga watoto na wake zao nyakati za usiku.

Polisi Kata ya Mwakata, Sajini Wilison Batiani, alisema wanapowakataa wanaofanya vitendo vya kikatili dhidi ya watoto na kinamama, baadhi ya wajumbe wa kamati za MTAKUWWA, wamekuwa wakilalamika na kudai wawaache jambo ambalo linawawia vigumu kufanya kazi.

Awali akitoa mafunzo hayo, Ofisa Ustawi wa Jamii Kiongozi kutoka halmashauri ya Msalala, Ignace Lufulila, alisema baadhi ya wajumbe wa MTAKUWWA wamegeuza matukio ya ukatili wa kijinsia kama fursa ya kujipatia kipato na wakati mwingine uamuzi umekuwa ukifanywa kimyakimya huku waathirika wakiendelea kuumia.

Alisema ikiwa kesi ya ukatili imefikishwa katika vyombo vya sheria, inakuwa imewakosesha ulaji, hivyo aliwataka kuhakikisha kila tukio linawasilishwa katika vyombo vya sheria.

HABARI KITAIFA

## Mikorosho milioni 15 sasa kupandwa

**Na Abdallah Bakari,** TUNDURU

BODI ya Korosho Tanzania (CBT) imegawa tani 107 za mbegu bora za korosho kwa wakulima wa zao hilo nchini kwa lengo la kuwezesha upandaji wa mikorosho milioni 14.9 katika mashamba mapya na uboreshaji wa mashamba ya zamani.

Lengo ni kufikia uzalishaji wa tani 700,0000 kutoka tani 300,000 za korosho ifikapo mwaka 2030.

Katika hafla ya kitaifa ya uzinduzi wa ugawaji wa mbegu bora za korosho iliyofanyika wilayani Tunduru mkoani Ruvuma mwishoni mwa wiki, Kaimu Mkurugenzi wa CBT, Francis Afred, alisema mbegu hizo zenye thamani ya shilingi 535 milioni zitagaiwa bure kwa wakulima wa mikoa 20 inayolima zao hilo.

"Tani hizi 107 za mbegu bora za korosho tumezinunua kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele na tutazigawa kwa wakulima wote wa korosho nchini kulingana na mahitaji yao...tani hizi zitatuwezesha kupamba miche mipya 14.9 milioni ikiwa ni zaidi ya asilimia 99 ya lengo la upandaji wa miche 1.5 milioni," alisema Alfred na kuongeza:

"Lengo kuu ni kuongeza uzalishaji kutoka tani 300,00 za sasa hadi tani 700,000 ...Ni wajibu kwa kila halmashauri kuwandaa wakulima wao ili mbegu hizi zifikie shambani kwa ajili ya kupandwa, ni imani yangu kuwa jitihada hizi za serikali zitainua kiwango cha uzalishaji za zao letu hili ambalo ni muhimili wa uchumi nchini."

Akizindua ugawaji huo, Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, aliwaagiza wakulima kutoziuza au kuzichoma mbegu hizo na kwamba kila mkulima atalazimika kuonesha shamba alilopanda mbegu hizo.

"Niupongeze mpango huu wa serikali kwani unakwenda kuinua tasnia ya korosho nchini, lakini niwaonye wakulima wenye tabia ya kuuza au kuchoma mbegu hizi, tutaonana wabaya," alisema Mtatiro katika hotuba yake iliyosomwa na Augustino Maneno, Kaimu Katibu Tawala Wilaya hiyo.

Alisema: "Upandaji wa mbegu hizi lazima uendane na matumizi ya kanuni bora za kilimo, sio suala la kupokea mbegu na kupanda bila kufuata maelekezo ya wataalamu hapana, ni lazima jitihada hizi ziende sambamba na kukiboresha kilimo chetu kiwe cha kisasa zaidi."

Mwakilishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kituo cha Naliendele ambao ndiye wazalishaji wa mbegu hizo, Saidi Mawenj, alisema mbegu hizo za kisasa ni muhimu kwa ajili ya mapinduzi ya kilimo nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Tunduru, Chiza Marando, alibainisha kuwa ugawaji wa mbegu hizo utafanyika kwa wakulima ambao wameandaa mashamba yao na kwamba zoezi hilo litatanguliwa na uhakiki wa mashamba.

# DC Ilala ataka wananchi kujitokeza kufanya usafi

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi Desemba 4, mwaka huu, kufanya usafi kwenye maeneo mbalimbali kwa kuwa ni muhimu kwa afya na mazingira yao.

Akizungumza na gazeti hili, alisema siku hiyo itazinduliwa kampeni ya usafi kimkoa katika Kata ya Kivukoni, na kwamba mgeni rasmi atakuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla.

Alisema suala la usafi wilayani humo ni la kimkakati na limepewa kipaumbele kutokana na umuhimu wake kijamii na kwamba ni muhimu likaanzia ngazi ya familia, mtaa, kata, wilaya, mkoa hadi taifa.

"Nitoe wito pia kwa kila kiongozi wa serikali za mtaa katika eneo lake achague eneo la kufanya usafi ambalo wananchi wote mnaombwa kushiriki siku hiyo ya usafi kuanzia ngazi ya familia, mtaa na kata ili kuyafanya mazingira yanayotuzunguka kuwa safi," alisema Ludigija.

Aliongeza kuwa suala la usafi litakuwa endelevu na utakuwa ukifanyika kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kwa kila mtaa kata na wilaya, pia alitoa wito kwa wadau ikiwapo kampuni za usafi kushiriki na kutoa vifaa vya usafi.

Aidha, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani Dar es Salaam, aliwataka wananchi kujiepusha na uzibuaji wa chemba unaosababisha majitaka kuingia katika mitaro jambo ambalo ni kinyume na sheria, na kwamba watakaobainika watachukuliwa hatua ikiwamo kufikishwa mahakamani.

"Nitoe tahadhari kwa wenye tabia hizo waache kwani lengo la kuhamasisha na kufanya usafi ni ili mazingira yetu yawe safi sasa mtu akiruhusu majitaka kuingia kwenye mitaro itakuwa michafu na itasababisha magonjwa ya milipuko jambo ambalo litahatarisha afya za watu," alitahadharisha Ludigija.

Pia alitoa agizo kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri maarufu daladala kuweka chombo cha kuhifadhia taka ndani ya gari na kuwapa maelekezo abiria kuwa wasitupe taka kiholela, ili mazingira yaendelee kubaki safi.

Alisisitiza kwamba abiria yoyote atakayeonekana akitupa taka nje ya gari alilopanda litapigwa faini, sambamba na mtembea kwa miguu, huku akibainisha kuwa adhabu yake ni faini laki 3 au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya TCC Plc, Paul Makanza, akizungumza katika hafla ya maadhimisho ya miaka 60 ya kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Dubai yawafungulia milango Watanzania vivutio utalii

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Jiji la Dubai katika Umoja wa Falme za Kiarabu imefungua milango kwa Watanzania kufurahia vivutio vya utalii vya jiji hilo.

Tamasha hilo lililopewa jina la 'AfroZons Dubai Soundoff ni mradi ambao umeratibiwa na Serikali ya Dubai kupitia Kituo cha Biashara, Masoko na Utalii (Dubai Tourism) kwa kushirikiana na Umoja wa Watangazaji maarufu wa radio wenye asili ya Afrika kutoka nchini Marekani (Afrozons Radio).

Katika tamasha hilo kwa upande wa Afrika litaratibiwa na watangazaji kutoka nchi za Nigeria, Ghana, Kenya, Tanzania, Angola, Zambia ambao kila mmoja ataungana na wasikilizaji wake kuelekea Dubai kwa safari ambayo imelipiwa kila kitu.

Akifafanua kuhusu mradi huo, Mtangazaji wa kituo cha Redio cha Clouds Fm, Meena Ally ambaye ndiye mwakilishi kutoka Tanzania aliyechaguliwa kushiriki tamasha hilo, alisema Afrozons inalenga kuutangaza muziki wa Afrika yaani Afrobeat.

Aidha, alisema kila mtangazaji wa nchi hizo atapata nafasi ya kwenda Dubai, lakini atapata nafasi ya kugawa tiketi tano ambazo zinawawezesha wasikilizaji wake kufika Dubai.

Amesema tiketi hizo zitafadhili safari nzima kuanzia usafiri, chakula, malazi, visa na matukio mbalimbali yatakayokuwa yanafanyika katika eneo hilo kama kutembelea vivutio mbalimbali.

Pia alisema kuna kampuni za usafiri wa anga Tanzania zimechaguliwa kutoa huduma ya usafiri kwa watu mbalimbali kuelekea Dubai kwa bei punguzo ambapo kwa safari ya mtu mmoja itakuwa kama dola za Marekani 400, lakini watapata fursa ya kutembelea maonyesha ya kibiashara nchini humo yanayofahamika kama Dubai Expo2020.

Aidha, mmoja wa wadau wa utalii nchini, Fahad Rajab Mwajasho ambaye ni mmiliki wa kampuni ya utalii wa ndani ya Unzip Tanzania, ametoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo kutokana na bei punguzo ya tiketi iliyotolewa na ufalme wa nchi za kiarabu.

Ofisa Mtendaji wa Kituo cha Biashara, Masoko na Utalii (Dubai Tourism), Issam Kazim, alisema zaidi ya watu 1,500 watashiriki tamasha hilo.

# Jamii yahimizwa kutoa taarifa za wanaofanyia ukatili watoto

**Na Elizabeth Zaya**

OFISA Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mpwapwa mkoani Ddodoma, Fadhili Molel, amesema bado kunahitajika nguvu kubwa ya kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu kutoa taarifa na ushirikiano wao kwa vyombo vya dola katika kushughulikia kesi zinazohusiana na masuala ya ukatili kwa watoto na wale wanaowapatia ujauzito.

Molel alitoa kauli wakati akizungumza na Nipashe mjini Mpwapwa kuhusu namna wanavyokumbana na changamoto ya kuwabaini wanaotekeleza vitendo hivyo kutokana na kukosa ushirikiano kutoka kwa wananchi au wazazi.

Alisema vitendo vya ukatili kwa watoto katika wilaya hiyo bado vinafanyika kwa wingi, lakini wanapofuatilia kwa ajili ya kuchukua hatua mbalimbali za kisheria, wamekuwa wakikosa msaada kutoka kwa wazazi au wananchi wenye taarifa.

"Kwa mfano hapa Mpwapwa tunapata taarifa nyingi sana za watoto kubakwa au kupewa ujauzito, lakini tunapambana kuchukua hatua kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya dola, tunakosa ushirikiano kabisa kwa wananchi au wazazi,"alisema Molel.

"Kwa mfano leo nimeshinda mahakamani kuna kesi ambayo tulikuwa tumeipeleka mahakamani, kuna kijana alimpatia ujauzito mtoto wa shule na mimi nilienda hadi kwa wazazi wake nikazungumza nao, tukakubaliana kwamba shauri hili lazima lifike mahakamani, lakini mwisho wa siku nimefika pale nawapigia simu wanasema wako njiani wanakuja, lakini mpaka muda wa mahakama unakwisha hawajafika."

Alisema kesi kama hizo mara nyingi wazazi wa pande zote mbili wamekuwa wakiitana na kumaliza wenyewe kwa wenyewe na hata kumtorosha mtuhumiwa kutoka kijiji au sehemu moja kwenda sehemu nyingine mbali ili kukimbia kesi.

"Na ndio maana tunasema huenda labda hawa wazazi na wananchi hawajafahamu athari za watoto wao kupatiwa ujauzito katika umri mdogo na kukatisha masomo yao au kufanyiwa ukatili, labda tuendelee kutoa elimu na hili halitakiwi kuwa la mtu mmoja, nguvu ya pamoja inahitajika, la sivyo hatuwezi kushinda,"alisema Molel.

Kwa upande wake, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mpwapwa, Deborah Maiko, alisema katika eneo hilo bado vitendo hivyo vya ukatili kwa watoto vinaendelea kufanyika, na kwamba bila jamii kubadilika na kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola, watoto wataendelea kuumizwa na kukosa haki zao za msingi ikiwamo kukosa elimu.




Meneja Mwandamizi wa Chapa ya Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo (kushoto), akizungumza katika uzinduzi wa kampeni mpya ya 'Maajabu Halisi na Coca-Cola' nchini Tanzania, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja Mkuu wa Shughuli za Biashara wa kampuni hiyo, Hellen Masumba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu waumini kumkataa askofu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAUMINI wa Kanisa la Makambako Christian Center MCC Halmashauri ya Mji Makambako Mkoa wa Njombe wameahirisha ratiba zote za ibada na kufanya maandamano, huku wakishinikiza kurejeshwa kwa mchungaji wao.

Wanadai mchungaji huyo kuondolewa kanisani hapo na Mwenyekiti wa Ushirika wa Makanisa Tanzania (TFC), na kwamba ameondolewa pasipo kufuatwa kwa katiba.

Wakizungumza na Nipashe waumini hao waliomba serikali kuingilia kati ili kumaliza mgogoro huo, huku wakieleza nia yao kuwa ni kuachana na ushirika huo pamoja na kurejeshewa mchungaji wao jambo ambalo mwenyekiti wa TFC anadaiwa kushindwa kulitekeleza.

"Mgogoro huu unasababishwa na mwenyekiti wetu ambaye anajiita askofu ni mtu ambaye hapendi kushirikiana na uongozi wa kanisa au waumini kwenye maamuzi hasa ili la kumtoa mchungaji, hatuwezi kuendelea nae kwa sababu licha ya kumlalamikia kwa barua kadhaa lakini anatupuuza," alisema Musa Kambo.

Naye Ester Jeremia alisema kuwa wao waumini hawana mgogoro na mchungaji wao isipokuwa mwenyekiti huyo ndio anakiuka katiba.

"Sisi ni kanisa huru linalojitegemea na kufanya maamuzi yake binafsi lakini kilichotufikisha hapa ni kutokana na kufukuzwa kwa mchungaji, askofu ametusababishia mgogoro mkubwa mpaka hatuna amani watu wa Makambako tunaomba serikali itusaidie, najua yupo Waziri wa Mambo ya Ndani pia yuko msajili wa vyama atusaidie watu wanatumia katiba isivyo sahihi," alisema Besta Luvanda.

Alijibu malalamiko hayo kwa njia ya simu Mwenyekiti wa TFC, Askofu Godfrey Malasi, alisema mgogoro huo ni wa muda mrefu tangu Julai mwaka huu.

"Limeshughulikiwa hapa sio leo tu lina mlolongo mrefu tangu mwezi wa saba, utaratibu mbalimbali umefanyika ila kwa sababu ni watu wa fujo walikuwa wanasimamiwa na vyombo vya usalama," alisema Malasi.

Malasi aliongeza: "Tulichoamua sasa tunaandika waraka wa amani kwamba wakitaka kuendelea pale wenyewe kama wanafikiri wana haki zote na sisi hatutawagusa tena ili wawe na amani, lakini katika utaratibu wale watu walichokifanya sio sahihi na kwa kuwa wameamua kutukana, sisi tumenyamaza Mungu ataamua mwenyewe."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issah, alifika kanisani hapo na kutoa wito kwa taasisi na vikundi kuwa na uwazi katika mifumo ya uendeshaji wa taasisi zao ikiwamo kuweka bayana taratibu walizojiwekea.

"Kwa hali kama hii na waumini walivyokuwa wengi, tumekuta kuna mabango yapatayo 40 na yote yakiwa yanapinga uamuzi wa askofu," alisema Kamanda Issah.

## Coca-Cola yaja na kampeni mpya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Coca-Cola Tanzania, imezindua kampeni mpya inayojulikana kama 'Maajabu Halisi'.

Kampeni hiyo kwa mwaka huu, itasherehekewa kwa namna tofauti na wasafiri wa usafiri wa umma kwenye mabasi na treni, ana kwa ana, ili kuwa kufurahia na wapendwa wao maeneo tofauti nchini wakati wa msimu wa sikukuu.

Kampeni hiyo inamkaribisha kila mmoja kusherehekea, kuungana na kuwainua watu kila siku, kuendana na hali ya maisha ya sasa duniani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Coca-Cola Kwanza Tanzania, Unguu Sulay, ndiye aliyebainisha hayo na kwamba kwa miezi 18 iliyopita mafunzo yalitolewa, miongoni mwake ni kufurahi pamoja nyakati za muhimu.

Alisema kutokana na changamoto wanazokumbana nazo kizazi cha sasa, kampuni hiyo imebuni namna bora ya kuishi maisha halisi na kufurahia sikukuu, badala ya kuegemea kidigitali pekee, mfumo ambao kwa asilimia kubwa umezoeleka.

"Tunapozindua kampeni hii ya 'Maajabu Halisi' Tanzania, dhumuni letu kuu ni kuwashirikisha na kusherehekea kwa pamoja nyakati muhimu na za kusisimua kwenye maisha yetu tofauti ya kila siku na watumiaji wa bidhaa zetu nchini kote, ili kuwainua na kuwaunganisha," alisema Sulay.

"Kwa zaidi ya miaka 100, dhima ya Coca-Cola, imekuwa ni kusambaza matumaini kampeni hii, imekuja kuendeleza ahadi hiyo. Tunaamini kwamba falsafa yake itaendana na watu wote duniani, kwamba wote tunaweza kuwa na nyakati za muhimu na za kusisimua katika maisha yetu halisi, iwapo tutajumuika na kushirikiana kwa pamoja."

Mkurugenzi huyo, alibainisha, kupitia kampeni hiyo watashirikishwa wasanii na wahamasishaji tofauti, lengo likiwa kuwainua na kuwaunganisha watu kwenye nyakati halisi na za kusisimua.

"Maajabu Halisi, imekuwa kampeni ya kwanza kuzinduliwa na Coca-Cola duniani kote tangu mwaka 2016, imezinduliwa pamoja na utambulisho mpya wa mtazamo kwenye chapa, ambayo itahusisha shughuli zote za kimasoko na kifungashio maarufu cha Coca-Cola.

"Kampeni hii pia itakuwa imebeba kampeni nyingine inayojulikana kama 'One Coke Away From Each Other,' ambayo imetengenezwa kwa ajili ya jamii inayohitaji kitu tofauti zaidi.

**Mkurugenzi Mtendaji wa Coca-Cola Kwanza Tanzania, Unguu Sulay, ndiye aliyebainisha hayo na kwamba kwa miezi 18 iliyopita mafunzo yalitolewa, miongoni mwake ni kufurahi pamoja nyakati za muhimu.**

2021 Afrika ilivyodhihirisha bara la migogoro, machafuko

Ukurasa 12



Ukurasa 14



# MWANAKANDANDA GEORGE WEAH Licha ya kuzaliwa, kukulia ufukara amekwama kusaidia maskini Liberia



# NDIVYO UNYANYASAJI KIJINSIA UNAVYOTAJWA KUTIKISA VYAMA

**Na Yasmine Protace**

MFUMO dume silaha inayotumiwa na baadhi ya wanaume kujikweza kwa hisia kuwa ndiyo wenye uwezo wa kufanya kila jambo kwa ufanisi na kuwatenga wanawake, unalalamikiwa kila kona safari hii, vyama vya siasa vikiwa mtuhumiwa namba moja.

Ndani ya vyama hivyo, unyanyasaji na ubaguzi unatajwa na hivi karibuni viongozi wanawake kutoka vyama 19 vya siasa, wanauibua kwa kina na kueleza namna unavyomkandamiza mwanamke kisiasa.

Wanazungumza katika mafunzo yanayolenga kuangalia umuhimu wa kutekeleza masuala ya kijinsia ndani ya vyama vya siasa, yanayoratibiwa na TGNP Mtandao na shirika la ULINGO.

Baadhi ya viongozi wanaeleza kuwa mfumo dume uliopo katika vyama hivyo unachangia wanawake kushindwa kupata nafasi za ukatibu mkuu au mwenyekiti wa chama lakini pia unawakandamiza hata wakishiriki mikutano wanatishiwa kunyang'anywa nauli na gharama walizolipwa.

### KUPOKONYWA POSHO

Mmoja wa washiriki jina na chama vinahifadhiwa analalamikia ukandamizaji wanawake uliokithiri ndani ya chama chao.

"Unaposhiriki semina au mafunzo kama hayo ukirudi ofisini uongozi unakulazimisha uchangie ulichokipata ili kiingizwe katika chama kulipia kodi ya pango..." anasema.

" Huo ni ukatili wa kiuchumi, viongozi wa juu wa chama wanaposafiri hawakatwi posho lakini sisi wanawake tunaambiwa pesa uliyoipata isaidie chama," anasema mshiriki huyo.

Anaongeza kuwa inafikia hatua ukienda semina unafuatiliwa ukipewa pesa viongozi wanataka wazichukue, wakati semina umeshiriki wewe. Anaongeza: "Vikao vinapofanyika wanawake wanashindwa kufanya maamuzi kwavile ni wachache. Lakini hata hao wachache wenye nafasi wanalazimika kusaka nauli kwenda katika mikutano hiyo na ziara za chama na wakati mwingine hawana kitu."



Dk. Ave-Maria Semakafu, akizungumza kwenye majukwaa ya harakati za usawa wa kijinsia. **PICHA MTANDAO**

Mshiriki mwingine analalamikia ukiukwaji mkubwa wa haki za wanawake akieleza kuwa ukitaka kufanya ziara wanakuruhusu lakini hakuna uwezeshaji wa pesa.

Wanataka kuangaliwa upya katiba za vyama ili kuwapa nafasi za juu za uongozi wanawake kwenye vyama ngazi za katibu na mwenyekiti ili uwiano uwe sawa.

Wanasema vyama vinakosea kutoa nafasi za juu za uongozi ki usawa wakiamini kuwa wanaume pekee ndiyo wenye uwezo na mwanamke hawezi kuongoza.

### WOGA KIKWAZO

Mshiriki mwingine jina tunalitunza pia, anasema woga walio nao wanawake unawakwamisha masuala mengi yanayowahusu.

"Kutokujiamini kunasababisha kushindwa kugombea, nafasi mbalimbali za ndani ya chama au kitaifa hata kwenye uchaguzi wa viongozi wa mitaa, udiwani,ubunge na uraisi inakuwa vigumu."

Washiriki hao wanasema vyama havina pesa na kutokana na kutofanya mikutano wanashindwa kupata wanachama wapya ,ambao wangenunua kadi na pesa zaidi zingeingia katika mifuko ya chama.

Wanasema hali ni mbaya ndani ya baadhi ya vyama, ikichangia kuwarudisha nyuma kwenye uongozi, kutoa maamuzi na kushiriki kwenye siasa za ndani.

Wanaiomba ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kabla ya kutoa usajili katiba ya chama ikaguliwe kueleza namna taasisi hiyo inavyoshirikisha wanawake.

Dokta Ave Maria Semakafu, Mratibu wa Ulingo Taifa, anasema sheria ya vyama inasema chama chochote kinachosajiliwa, lazima kiwe na masuala ya kijinsia .

"Pamoja na kuwapo kwa sheria hiyo, baadhi ya vyama viongozi wa juu ni wanaume hakuna ushirikishaji wanawake, hali hiyo inachangia wanawake kushindwa kushiriki na kufanya maamuzi," anakumbusha na kuwataka kurejea katiba inayosema binadamu wote ni sawa.

" Kama sheria inasema binadamu wote ni sawa, inakuwaje nafasi za juu za uongozi usawa uwekwe pembeni," anahoji na kuongeza kuwa katika utambulisho wa viongozi wa vyama, mara zote wanaojitambulisha ni wanaume.

Dokta Ave Maria, anaongeza kuwa ukiangalia hata takwimu za dunia zipo nchi 24 pekee zenye viongozi wanawake wakuu wa nchi au wakuu wa serikali.

"Mawaziri duniani kote wanawake ni asilimia 21. Na ni nchi nne pekee zenye wabunge wanawake zaidi ya asilimia 50."

Ave-Maria, anazungumzia miaka 60 ya Uhuru, akisema taswira imebaki ile ile ya kuwapo na wanaume kazi za juu za uongozi huku wanawake wakiwa chini.

" Tunataka haki ya usawa iwapo katibu mkuu ni mwanamke, mwenyekiti awe mwanaume," anashauri.

Lilian Liundi Mkurugenzi Mtendaji TGNP Mtandao, anasema ni lazima kuwapo na uwakilishi wa wanawake katika uongozi na ilani zinaitaja ajenda ya 50 / 50 lakini bado kuna mapengo.

Anakumbusha kuwa uongozi utakuwa na tija kama kunakuwapo na usawa na kwamba ajenda ya mwanamke ni ajenda ya kitaifa na ndiyo turufu (karata inayotawala mchezo) ya ushindi.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa Zanzibar, Mohamed Ally Ahmed, anasema mafanikio ya usawa wa kijinsia Tanzania yatafanikishwa na wanawake kujipambania wenyewe.

" Sheria ya vyama iboreshwe ili kuelekeza

vitambue na kumpa mwanamke fursa katika ngazi za juu za uongozi," anasema.

Grace Haule Katibu wa UWT, Mkoa wa Dar es Salaam, anasema kupitia mfumo wa vyama vingi ,wanawake wa CCM wanapata haki katika uchaguzi.

Anaongeza kuwa asilimia 30 imetengwa kwa ajili ya wanawake na lengo la CCM ni kuona wanawake wanajitokeza katika kugombea ubunge majimboni.

Anaongeza kuwa vyama vingine navyo vinatakiwa kutenga nafasi kwa ajili yao na kuwaachia nafasi za kugombea majimboni.

Anaongeza kuwa uchaguzi wa 2025 Rais Samia Suluhu Hassan, anataka aungwe mkono na ikiwezekana iwe ajenda ya kudumu.

Anaongeza kuwa idadi ya wanawake nchini ni asilimia 53 hivyo wanaweza kushika nafasi za juu na kuwataka waendelee kuwatengea nafasi.

Saumu Rashid kutoka ULINGO anasema wanawake wengi hawajui sheria jinsi zinavyowalinda.

Anaongeza kuwa viongozi wanawake wanatakiwa kujifunza sheria za vyama vya siasa ili ziwanufaishe na kuwaendeleza kisiasa na uwe mwanzo wa ushiriki mkubwa wa kimafanikio kufikia 50/50.



Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, ambapo nchi yake imetumbukia kwenye mapigano ya kimajimbo na kusababisha mkwamo kisiasa na kiuchumi. **PICHA: MTANDAO**

# 2021 Afrika ilivyodhihirisha bara la migogoro, machafuko

**Na Christina Mwakangale**

MIGOGORO inayoendelea barani Afrika katika kanda zote kaskazini hadi kusini, magharibi na mashariki, unalifanya bara hilo kuibua maswali mengi, huku likionekana kuwa halina dhamira ya kujikomboa na umaskini, licha ya utajiri wa rasilimali zilizopo.

Changamoto hiyo inatokana na ukweli kuwa maendeleo ya taifa lolote hutegemea amani, utulivu na kuheshimu haki za raia.

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Gwandumi Mwakatobe, akizungumza na Nipashe kuhusu vurugu za kisiasa kwa nchi nyingi za Afrika, anasema nchi zilizo kwenye migogoro zimekuwa zikiachwa yatima, licha ya kuwapo jumuiya za kikanda.

"Afrika Magharibi nchi nyingi zina uongozi wa kimapinduzi japo zilitulia kidogo lakini sasa migogoro inajirudia mara kwa mara. Mapinduzi yanajirudia pia hata kwa nchi ambazo zinakabiliwa na vitisho vya ugaidi."

Anataja nchi za Mauritania, Mali, Burkina Faso, Chad, Niger, Msumbiji na Ethiopia kuwa ni mojawapo ya mataifa yenye mitafaruku kisiasa.

> "Afrika Magharibi nchi nyingi zina uongozi wa kimapinduzi japo zilitulia kidogo lakini sasa migogoro inajirudia mara kwa mara. Mapinduzi yanajirudia pia hata kwa nchi ambazo zinakabiliwa na vitisho vya ugaidi."

Anasema mbaya zaidi nchi hizo zinapitia mengi kwa sasa mfano janga la corona, umaskini, vita vya wenyewe kwa wenyewe yote yanazidi kurudisha nyuma bara la Afrika, akisema ambako kuna utajiri wa asili ikiwamo mafuta.

"Nchi hazijapona na COVID-19 wanapambana na mambo mengi kwa wakati mmoja, sababu za migogoro ni kubwa tatu, utajiri, ung'ang'anizi mamlakani, jumuiya za kikanda kuchelewa kutatua migogoro na umoja duni baina ya nchi na nchi," anasema Gwandumi.

Anasema barani Afrika viongozi ambao hawatarajii kuachia madaraka ni sababu ya migogoro huku wakibadili katiba na kusababisha wakati mwingine majeshi kuingilia kati.

"Mfano ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki baadhi ya viongozi walibadili katiba, lengo ni kujilinda wasing'oke madarakani. Nchi nyingi za viongozi wengi hata Alpha Conde wa Guinea pia alibadili katiba," anakumbusha Gwandumi.

> "Nchi zenye migogoro zinaachwa yatima, hadi jumuiya za kimataifa za nje ziingilie, viongozi waasisi walitamani tuwe na fedha na serikali moja. Hawa watu walipokuwapo waliitikia mapema, kila jambo." anasema

**KUWAPO KWA UTAJIRI**

Gwandumi anasema nchi za Afrika Magharibi karibia zote zina utajiri wa mafuta, ikiwamo Mali na Nigeria inayoongoza kwa uzalishaji nishati hiyo barani.

"Nigeria wana mafuta na wanaofaidika nayo ni wachache. Kaskazini kuna ukame na migogoro mikubwa ipo kwa wakulima na wafugaji, kila mmoja anadai upande wake haunufaiki," anaeleza.

"Viongozi wa nchi hizo wanachukua muda mrefu kutatua matatizo.

Jumuiya za Kikanda mfano ECOWAS , ECOMOG Afrika Magharibi zinachelewa kutatua migogoro." Anaongeza Gwandumi.

Anautaja hata Umoja wa Afrika (AU) kuwa unashindwa kuingilia na kutatua changamoto za bara hilo mara moja.

Anasema jumuiya za kikanda zina majeshi na wanadiplomasia lakini hakuna ututuzi wa mapema wa migogoro.

"Ethiopia inapigana yenyewe na majimbo yake yanayo asi, wameachwa kama yatima hadi msuluhishi atoke nje ya bara , ndiyo aje kuingilia mgogoro na kuwasuluhisha, naweza kusema AU, umoja wa kikanda unashindwa kushughulikia matatizo ya Kiafrika mapema," anasema mchambuzi huyo.

**MIAMBA YA AFRIKA**

Gwandumi anasema anawakumbuka viongozi waasisi wa mataifa ya Afrika, ikiwamo Mwalimu Julius Nyerere, Kwame Nkrumah, Nelson Mandela, ambao walikuwa mstari wa mbele katika kutatua migogoro ya Waafrika kwa juhudi zao wenyewe kabla ya utegemezi wa kigeni.

"Jirani yako akiwa na vita hata wewe hauko salama. Msumbiji tangu mwaka 2017 ina vita lakini hivi sasa ndiyo mataifa ya Jumuiya ya Umoja wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yanaungana kuisaidia."

"Nyumba ya jirani inapoungua nenda kazime moto, sababu unaweza kuhamia nyumbani kwako," anaeleza Gwandumi.

"Nchi zenye migogoro zinaachwa yatima, hadi jumuiya za kimataifa za nje ziingilie, viongozi waasisi walitamani tuwe na fedha na serikali moja. Hawa watu walipokuwapo waliitikia mapema, kila jambo." anasema

Anakumbusha kuwa Nyerere aliitikia wito kusuluhisha Burundi na Nelson Mandela pia. Viongozi wengi wa leo wanang'ag'ania madaraka.

Inabidi waungane, waonyeshe, uwajibikaji wa pamoja na huo ndiyo msingi.

Anasema, Nkrumah aliwahi kusema Afrika itakuwa huru iwapo kila mmoja atakuwa huru, akisema iwepo sera moja, na kutoyategemea zaidi yaliyokuwa makoloni kuja kutatua.

**KUJITATHIMINI KI-APRM**

Balozi Mindi Kasiga, kutoka sekretarieti ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Afrika (APRM), akizungumza kwenye mkutano wa pamoja uliokutanisha taasisi mbalimbali, hivi karibuni, anasema kutokuwapo kwa utawala bora barani Afrika ni kikwazo cha maendeleo.

"Tusisubiri kutoka nje au Umoja wa Mataifa (UN), utuambie hatuna utawala bora, Afrika tujitathmini wenyewe. Utawala bora hauwezi kufanana na nchi za nje, mfano China, Marekani, tufanye juhudi zetu kama Waafrika," anasisitiza.

## SIKU 16 ZA KUPINGA UKATILI KIJINSIA

# Ndiyo Zanzibar isiyonyanyasa

## ■Ni ujio wa Mahakama ya kesi za udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**



Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mwiji Talib Haji. **PICHA: MTANDAO**

KUANZISHWA Mahakama Maalumu ya Kesi za Udhalilishaji Zanzibar, kumewaamsha wanafamilia na wadau wengine wengi kuongeza juhudi za kupambana na vitendo vya udhalilishaji hasa kwa watoto.

Mwamko huo unatoa matumaini ya kusaidia kupunguza au kutokomeza vitendo hivyo ambavyo kasi yake ilikuwa kubwa sehemu nyingi Unguja na Pemba katika miaka ya karibuni.

Mahakama hiyo iliyoanza kufanyakazi rasmi Julai mwaka huu baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuagiza ianzishwe, kufuatia kushamiri vitendo hivyo na kwamba hadi sasa kesi 194 zimeripotiwa mahakamani Unguja na Pemba.

Miongoni mwa kesi hizo 181 zilizofunguliwa mahakamani, mashauri ya ubakaji yanaongoza ambayo ni 106 yakifuatiwa na kesi za ulawiti 29.

Kwa mujibu wa Mahakama Kuu mashauri yenye utambulisho 'K/Kubaka' ni inatambulisha kesi za kujaribu kubaka wakati 'K/Maumbile' ni kuingilia kinyume cha maumbile na 'K/Maharimu' ni kumwingilia kimwili mwanamke ambaye huwezi kuoana naye kama dada yako, mtoto wa kumzaa au wa ndugu yako wa kuzaliwa pamoja.

**MAELEZO WAATHIRIKA**

Asha Juma (si jina halisi) ni mmoja ya wahanga wa kesi hizo ambaye mtoto wake mwenye miaka 11, anasema uwepo wa mahakama hiyo maalumu ya udhalilishaji imepelekea kesi yake kwenda kwa haraka na mshtakiwa kutiwa hatiani na kufungwa miaka 30 jela.

Anasema mtoto wake alifanyiwa kitendo hicho mwaka jana na kesi hiyo ilikuwa ikisuasua lakini baada ya kuanzishwa kwa mahakama maalumu shauri limekwenda kwa haraka na hatimaye haki imepatikana.

Mama huyo anazipongeza taasisi za kutetea haki za wanawake na watoto , Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar akisema kilimpatia elimu pamoja na mtoto wake jinsi ya kujiamini na kutoa ushahidi mahakamani.

"Naipongeza TAMWA kabla ya kesi hii kutolewa hukumu ilitupa elimu tukiwa na wahanga wenzetu wa vitendo hivi kutuelimisha namna ya kujiamini na kutoa ushahidi mahakamani na kutujengea ujasiri mkubwa,"alisema.

Anasema awali kabla ya kesi hiyo kutolewa hukumu alikuwa akipata vitisho kutoka kwa familia ya mshtakiwa wa kesi hiyo kutokana na msimamo wake wa kukataa kesi hiyo kumalizwa katika ngazi ya familia.

Anaeleza kuwa baada ya kutokea tukio hilo familia ya mshtakiwa ilimfuata ili kumpa kiwango kikubwa cha fedha ili kuifuta licha ya kufikishwa katika vyombo vya sheria lakini hakukubaliana nao.

"Kwa kuwa mshtakiwa wa udhalilishaji ni jirani yangu familia yake ilitaka kunikabidhi kitita cha fedha ili kesi hiyo niifute lakini nilikataa na kutaka haki itendeke na nashukuru hukumu imepatikana na kwa sasa mshtakiwa yupo jela,"anasema.

**MAHAKAMA**

Katika ufuatiliaji wa kutathmini kesi za udhalilishaji mahakamani kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu zimefunguliwa kesi 22 katika Mahakama ya Mkoa wa Kusini iliyopo Mwera, nyingine 14 katika Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja, kesi 77 Mahakama ya Mkoa wa Mjini Unguja.

Hakimu wa Mahakama Mkoa Mwera, Khamis Ali Silima anaiambia Nipashe kuwa kesi 16 zimeshamalizika na kuhukumiwa kati ya Julai hadi Septemba mwaka huu.

Aidha, nyingine tano (5) zimemalizika na hukumu kutolewa katika Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwa mujibu wa Hakimu wa Mahakama hiyo Mohammed Subeit na kesi saba zimeshahukumiwa na Mahakama ya Mkoa Vuga, anaeleza Hakimu Yesaya Kayange .

Mahakimu hao wanasema miongoni mwa kesi hizo zipo zilizotolewa hukumu kwa muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja wakati nyingine zilitolewa baada ya muda mfupi zaidi.

> "Kumalizika kwa kesi mahakamani hakuna muda maalumu uliowekwa na sheria, bali upo muongozo wa muda maalumu kwa kesi maalumu kuanza kusikilizwa mashahidi ndani ya miezi mitatu na kufikia hukumu au kufutwa au kumuachia mshitakiwa huru," anasema Silima Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja.

"Kumalizika kwa kesi mahakamani hakuna muda maalumu uliowekwa na sheria, bali upo muongozo wa muda maalumu kwa kesi maalumu kuanza kusikilizwa mashahidi ndani ya miezi mitatu na kufikia hukumu au kufutwa au kumuachia mshitakiwa huru," anasema Silima Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja.

Anasema moja ya sababu ambayo inapelekea kesi kusikilizwa kwa haraka ni jinsi mashahidi wanavyopatikana kwa wingi kwenda kutoa ushahidi na sababu nyingine ni uchunguzi kufanyika haraka kwa vile polisi hawachukui muda mrefu kukamilishwa upelelezi. Mrajisi wa Mahakama Kuu Zanzibar, Muhamed Ali Shein, anasema kuwepo kwa mahakama maalumu kutapunguza tatizo hilo kwa sababu chombo hicho kina uwezo wa kuwapa adhabu wanaokataa kutoa ushahidi.

Anaitaka jamii kuwa na ushirikiano inapotakiwa kutoa ushahidi ili kesi hizo kupatiwa hukumu zinazostahiki kwa sababu bila ya ushahidi watuhumiwa wa kesi hizo hawatatiwa hatiani.

Anaeleza kuwa kibano hicho hakitakuwa kwa mashahidi watakaokataa kufika mahakamani bali pia kwa hakimu ambaye hatafika mahakamani bila sababu za msingi kusikiliza kesi hizo.

Anawataka mahakimu kuelewa kwamba wanawajibika kufika mapema mahakamani na kuonya kwamba atayeshindwa kuwajibika atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mrajisi huyo anaongeza kuwa kesi hizo ni matokeo ya kuporomoka kwa maadili, matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii na malezi duni kwa baadhi ya familia.

**MAELEZO YA DPP**

Anasema katika kipindi cha miezi sita kuanzia Aprili hadi Septemba mwaka 2021, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) imepokea majalada ya kesi za ubakaji na ulawiti 405 kwa Unguja na Pemba .

Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja unaongoza kwa kuwa na kesi 222, Kaskazini Unguja 60, Kusini Unguja 34, Kusini Pemba 54 na Kaskazini Pemba 35.

Anaongeza kuwa kuna mwamko mkubwa wa wananchi kuripoti matukio ya udhalilishaji katika vyombo vya sheria.

Anasema licha ya mwamko huo lakini kuna changamoto kwa wahanga na mashahidi wa kesi za ukatili kukataa kutoa ushahidi mahakamani.

Wakati hayo yakitokea Ofisi ya DPP hupokea maombi mengi ya kufuta kesi kutoka kwa jamii.

**MAPENDEKEZO:**

Ili Mahakama Maalumu ya Udhalilishaji itoe hukumu kwa haki na wakati wanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto wanapendekeza elimu zaidi.

Fatma Juma msaidizi wa sheria anapendekeza elimu zaidi itolewe kwa wananchi na wafundishwe umuhimu wa kufika mahakamani kutoa ushahidi sahihi.

Pia anasema jamii ielimishwe namna muhali (kuoneana aibu) kunavyovuruga kesi na kunyima haki kwa anayetendewa jinai hiyo.

Hakimu Jesaya Kayange, kutoka Mahakama ya Vuga anataka kufanyike marekebisho ya sheria ya mtoto ili umri wa mtoto uwe na kikomo cha miaka 14 na siyo 18.

Anasema kutokana na kuonekana kesi nyingi zinazoripotiwa mahakamani huanzia na watoto wa miaka 15 ambao tayari wanajitambua.

"Jamii ielimishwe umuhimu wa kuendelea na kesi bila ya kukatisha njiani na familia ziache kutafuta suluhu nje ya mahakama,"anasema.

Dokta Mzuri Issa Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, anasema elimu itolewe kwa umma kuacha kutoa talaka ovyo na tatizo kubwa limeonekana wazazi wanapoachana watoto hukosa matunzo na hivyo kushawishika na kufanyiwa udhalilishaji.

Aidha, anasema familia zichukue wajibu wake wa kuwalea na kuwatunza watoto ili kuepukana na udhalilishaji wa ubakaji, kulawiti na kutoroshwa.

## MWANAKANDANDA GEORGE WEAH

# Licha ya kuzaliwa, kukulia ufukara amekwama kusaidia maskini Liberia

## ■Walalahoi majalalani wanalia amewaangusha

NA GAUDENSIA MNGUMI



Rais wa Liberia George Weah. **PICHA: MTANDAO**

VIONGOZI wengi wa Afrika wana historia ya kuanzia majukumu ya uraisi kutoka kwenye taaluma za siasa. Au wengi wanakuwa ni zao la wanasiasa . Labda wawe majenerali wanaoingia ikulu kwa mtutu.

Kwa George Weah, Rais wa Liberia haikuwa hivyo. Ni mwanamichezo, akiibuka kutoka kwenye uwanja wa soka, akicheza kabumbu au kandanda kitaifa na kimataifa.

Mwanasoka huyo, Januari 2018 alikula kiapo cha kuiongoza Liberia akiahidi kufanya maboresho na mabadiliko makubwa kiuchumi ili kujenga taifa jipya lenye mafanikio, kwa vile wengi ni maskini na maisha yao ni majalalani.

Wakati huo nyota wa soka George Weah, akitamani ikulu, aliona mambo pengine yangewezekana, lakini hali ni ngumu, urais si kama kuliona lango la timu pinzani na kupachika goli. Ni mlima mgumu na mrefu kuupanda

Kama angefanya mambo mazuri pengine angechukuliwa kama shujaa kutoka kwenye uwanja wa mpira hadi ikulu na kufunga bao la kisigino kwa kuboresha uchumi, maisha na kuiweka Liberia kwenye ramani ya nchi zenye uchumi unaokua kwa kasi duniani.

Mambo ni magumu wapiga kura hasa vijana waliompa Weah ushindi wa kishindo wana hali mbaya na maisha yamezidi kuwa duni kutokana na uongozi wake kushindwa kupambana na kukomesha rushwa kubwa na ufisadi .

"Ninamsihi Rais wangu asikilize sauti za watu maskini ambao walimpigia kura na kuwezesha mipango yake ya kuwa rais leo," anasema Mark Williams ( 23) mjasiriamali anayeuza mashine za kupiga chapa 'typewriter' kwenye jiji kuu la Monrovia.

"Wapigakura tuliamini kuwa kama tukimchagua Weah kuwa rais wetu atatuangalia na kutujali sisi maskini. Anafahamu nini kinachozungumziwa kwenye kusota na kuhangaika au kuwa mlalahoi kimaisha ,".

Mjasiriamali huyo anayasema hayo akitaja namna Rais wa Liberia alivyozaliwa, kukulia na kuishi katika mazingira magumu na kupitia utoto wenye shida nyingi ndani ya mitaa ya majalalani ya watu maskini katika jiji la Monrovia, kabla hajajipatia sifa za kimataifa akitajwa na kusifiwa kuwa mchezaji bora wa kandanda duniani kwenye miaka ya 1990.

"Tunakubali kuwa aliingia nchi ikiwa hoi, uchumi ulipooza lakini alikuwa na wajibu wa kuurekebisha alitaka na kuahidi kuutimiza wajibu huo,"

Weah alichukua nchi ikiwa na uchumi mahututi , ulioumizwa na kuporomoka, bei za mpira na chuma ambazo ni bidhaa kuu zinazouzeba uchumi wa Liberia, ebola nayo iliimaliza nguvu nchi hiyo kati ya mwaka 2014 hadi 2016 na kuongeza zaidi maumivu kwenye uchumi wa taifa hilo ambao asilimia 80 ya raia wake wanaishi chini ya dola 1.25 (sawa na Shilingi 2,875) kwa siku.

Rais Weah anapoingia madarakani anaahidi kuugeuza mwelekeo huo na kuleta maisha mapya kwa kila maskini akianza na kukomesha rushwa , kuongeza uwekezaji wa kigeni na kuwapatia ajira zaidi na shughuli za kuboresha maisha ya masikini walio wengi.

Lakini miaka mitatu ndani ya muhula wa miaka sita ya urais hana kikubwa cha kutambia. Kwa mujibu wa AZAKI za Liberia zinazofuatilia utendaji wa Weah zikirejea ahadi zake kwenye uchaguzi, ameangukia pua.

### RUSHWA IMEMWELEMEA

Katika Ripoti yake ya Januari 20 'taasisi ya Naymote Partners for Democratic Development'

> "Wapigakura tuliamini kuwa kama tukimchagua Weah kuwa rais wetu atatuangalia na kutujali sisi maskini. Anafahamu nini kinachozungumziwa kwenye kusota na kuhangaika au kuwa mlalahoi kimaisha ,".

inamtaja Rais Weah kuwa ametimiza ahadi saba kati ya 92 alizowaahidi wapigakura na kati ya hizo tano alizikamilisha wakati wa kipindi cha mwaka wa kwanza ikulu .

Ahadi hizo ni pamoja na kupitia mitaala ya elimu ya nchi hiyo, kupitisha sheria ya ardhi iliyokuwa inahitajika kwa miaka mingi na sheria ya kutoongeza mishahara ya viongozi wakuu serikali ambayo aliibakiza kuwa dola 7,800 (sawa na Shilingi 18) kwa mwezi.

Baadhi ya ahadi nyingine kiuchumi ni kupunguza kodi ya bidhaa zinazoagizwa nje na za bidhaa muhimu, kukarabati na kuboresha miundombinu ya barabara na kuanzisha mpango wa mikopo kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo. Lakini serikali yake imeshindwa kufanyiakazi ahadi kubwa iliyojitangazia.

"Hakuna kikubwa kilichofanyika kwenye ahadi zake za kuongeza uwajibikaji na utendaji kazi kwa ufanisi na kukabiliana na rushwa",AZAKI zinasema.

Aliahidi kutunga sheria na taasisi za kuikabili rushwa, kuwachukulia hatua mafisadi, kudhibiti na kukomesha rushwa kwenye sekta za umma na kuzishitaki kampuni zinazohusika na ufisadi na mambo mengine ya kutoa na kupokea rushwa kwenye zabuni za serikali na kwingineko na kudhoofisha uchumi na utendaji bora serikalini.

### KASHFA NZITO YA NOTI

Uchumi wa Liberia umedhoofu, mfumuko wa bei sasa ni asilimia 30 , mishahara ya watumishi wa umma inachelewa kupindukia, idadi ya wanaompinga inaongezeka kila siku.

Mamia ya watu walikusanyika jijini Monrovia kumpinga na kumlalamikia na serikali kulazimika kutumia jeshi la polisi, mabomu ya machozi na maji ya kuwasha kuwatawanya.

Serikali ya Weah inakabiliwa na tuhuma ikikabiliwa na kashfa ya kuchapisha noti za benki zenye thamani ya dola milioni 100 (sawa na Shilingi trilioni 2.3) lakini hazikuonekana popote ikiwa ni kashfa kubwa zaidi ya kiuchumi.

Kilichoongeza hasira ni uchunguzi kubaini kwamba madai hayo hayana ukweli na Benki Kuu ya Liberia ikiagiza sarafu mpya kabla ya kupata kibali cha bunge wala kupata vibali vingine muhimu vya kufanya hivyo, na kulazimika kutumia fedha nyingine nyingi zaidi kuliko za awali.

"Weah alidhani kuongoza nchi ni sawa na kucheza soka," anasema Robtel Neajai Pailey, mchambuzi wa kisiasa na kuongeza . "anakosa mbinu na njia za kuwa rais bora lakini umaarufu wake na uwezo alio nao ungemsaidia kupata timu bora ya viongozi lakini hakufanya hivyo badala yake ameruhusu kuendelea kushauriwa na washauri wabovu na kupokea maelekezo yake."

Anaongeza : "Walaiberia wanaona wanataka kugoma kutaka mambo makubwa na mabadiliko sababu hali iliyopo inawaumiza mno ."

### 'NIVUMILIENI KIDUCHU

Katika ujumbe wake wa mtandao wa facebook, Weah anawaambia Walaiberia nafahamu watu wamekereka zaidi hakuna furaha "lakini safari haikuwa rahisi naomba mshikamano imara na madhubuti na uungwaji mkono unaodumu".

Weah anaahidi kuendelea kukabili ufisadi ambao umeota mizizi kwenye jamii kubwa na kutangaza sheria mpya ya kuipa mamlaka na nguvu zaidi Tume ya Liberia ya Kupambana na Rushwa.

Kuna wakati alihutubia taifa na kusema "Naona mnakosa kabisa subira ninaona mlivyokosa na kushindwa uvumilivu Nawaombeni nipeni tena nafasi . Nivumilieni. Nijaribuni tena kwa kunipa nafasi kidogo nitarekebisha magumu haya."



HABARI DODOMA

# Askofu ataka kuipa serikali ushirikiano

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, amewataka viongozi wenzake kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali ili kuimarisha amani na mshikamano ndani ya jamii.

Dk. Chande alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na viongozi wa jumuiya hiyo ngazi ya kata na wilaya kwenye semina elekezi iliyofanyika wilayani Kondoa mkoani Dodoma.

Aliwataka kufanya kazi zao kwa weledi na kwa bidii, huku wakishirikiana na serikali ili kuimarisha mshikamano na amani iliyopo ndani ya nchi na kwa jamii.

Mwenyekiti huyo pia aliwataka viongozi hao wa maaridhiano kuhakikisha wanatoa elimu elekezi kwa jamii inayowazunguka ili waone umuhimu wa kulinda amani iliyopo katika taifa la Tanzania.

Alisema kuwa wao kama viongozi wanawajibu mkubwa wa kuwafikia wana jamii kwa kuwaelimisha ikiwa ni pamoja na kuwasisitiza kufanya kazi kwa bidii na malengo ili kuondokana na umaskini.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kondoa, Andrea Ng'hwani, alisema kuwa jumuiya ya maaridhiano ina nafasi kubwa katika kuchangia kutoa elimu ya uelewa kwa jamii inayowazunguka kwa kushirikiana na serikali ili amani iliyopo iweze kudumu ndani ya nchi.

Alisema kuwa serikali kwa kushirikiana na jumuiya ya maridhiano wanaweza kuwa chachu katika kuelimisha wanajamii na wao wakawa mabalozi wazuri wa kulinda amani hiyo.

"Hivyo basi niwaombe nyinyi viongozi kuanzia ngazi ya mkoa hadi vitongojini, endeleeni kuelimisha jamii katika suala zima la kuilinda hii amani ambayo kwa baadhi ya nchi za wenzetu hawana zaidi ya mapigano,"alisema.

# TAMISEMI yafunguka uhamisho wa watumishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imerudia msimamo wake kuwa imesitisha uhamisho kwa watumishi wa umma wanaotaka kuhamia mijini na kukataa kuishi vijijini.

Aidha, imesema kuwa badala yake itaendelea kutoa nafasi za kubadilishana vituo vya kazi kwa watumishi pale inapobidi.

Waziri wa TAMISEMI, Ummy Mwalimu alibainisha hayo juzi jijini hapa wakati wa mahafali ya 13 ya Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI).

Ummy, alisema uamuzi huo unatoa nafasi kwa wananchi wa pembezoni kupata huduma wanazostahili ikiwamo elimu na afya. Alisema, maeneo ya vijijini kuna uhaba mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali kutokana na watumishi wengi kukimbilia kufanya kazi mjini na kwamba ili kumaliza tatizo hilo lazima wahitimu wote wawe tayari kuajiriwa na kupelekwa sehemu yoyote yenye uhitaji.

"Nimesitisha na nitaendelea hivyo mpaka tutakapofanya msawazo wa watumishi lazima niangalie kwa nini Ukerewe kuna walimu 100 wakati Kinondoni kuna walimu 2,000 tutaangalia mahitaji na waliopo ili kufanya maamuzi sahihi wakati wa kuhamisha," alisema Ummy.

Aidha, alisema ili kuwapa hadhi wanayostahili watumishi, serikali imedhamiria kuboresha mazingira ya vijijini ikiwamo kuanzisha shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia ili kuwapa fursa watumishi wanaohitaji watoto wao kusoma katika shule hizo, kitu kitakachosaidia kuacha kutamani kuishi mjini.

Alisema ili kukidhi mahitaji ya ajira nchini, serikali itatoa kipaumbele cha ajira kwa wahitimu walio tayari kufanya vijijini, huku akiwataka wanachuo wa chuo hicho wanaomaliza muda wao kujiandaa kisaikolojia kuishi maeneo yoyote watakapo pangiwa ili kuisaidia jamii.

"Mnapopata ajira muwe tayari kwenda kufanya kazi kwenye halmashauri za pembezoni na sio mkishapata tu mnaanza kuomba uhamisho kurudi mjini, lazima mjifunze maisha ni popote mnapaswa kuridhika," alisisitiza.

Aidha, alisema Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaendelea kuajiri wataalamu wanaohitimu LGTI kwa kuwa wamepikwa kumika vyema kwenye Serikali za Mitaa.

"Lazima tuwe wakweli kwa sasa serikali itatoa kipaumbele cha ajira kwa wahitimu walio tayari kufanya kazi Halmashauri za Vijijini ambapo kuna mahitaji makubwa ya watumishi wa kada mbalimbali.

"Watu wa kijijini pia wanahitaji huduma zenu, hivyo watumishi wanahitajika kwenda kufanya kazi maeneo hayo na sio kung'ang'ania kubakia mjini wakati wote, kila mtu anataka Dodoma Jiji, Kinondoni, Arusha Jiji, Mwanza Jiji nani akae Mpimbwe, Uvinza, Kilindi, Rufiji."

Kadhalika, alisema serikali itaendelea kuboresha na kutatua kero zilizoko chuoni hapo ili kuboresha huduma za kijamii na kuongeza umakini wa masomo kwa wanachuo hao.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Chuo hicho, Prof. Joseph Kuzilwa, aliiomba serikali kuwezesha ujenzi wa barabara ya Ihumwa hadi Hombolo kwa kiwango cha lami ili kufikika kwa urahisi chuoni.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Mpamile Madale, alisema chuo kinakua siku hadi siku na kuongeza udahili ambapo wanafunzi waliohitimu mwaka 2021 ni 6,021.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jana, kuhusu ufunguzi wa kitaifa wa maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, utakaofanyika kesho katika Mji wa Serikali Mtumba. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Uswisi yataja dawa ya kumaliza umaskini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uswisi, Patricia Danzi, amesema jitihada ndio njia pekee ya kumaliza umaskini.

Danzi, alisema hayo juzi wakati alipotembelea wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika kijiji cha Wilunze Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

"Nimefurahi wanufaika hapa wanasema kwa uwazi sana, mara nyingi ni vigumu kuongea kuhusu maisha yako, lakini mkiwa na jitihada katika kufanya kazi mtajitoa kwenye hali ya umaskini," alisema.

Aidha, alisema kuna mawazo mazuri ndani ya Afrika yanayotakiwa kufanyiwa kazi na Sweden ambayo ni kama mafuta yanayowekwa kwenye mnyororo wa baiskeli ili iende.

"Kabla ya kuja hapa tulikutana na Rais Samia Suluhu Hassan na aligusia sana masuala ya maendeleo na tulimwahidi kuwa tutaendelea kushirikiana na Tanzania," alisema.

Kwa upande wake Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Didier Chassot, alisema Uswisi na Tanzania wamekuwa na mahusiano mazuri na sasa wanasherehekea miaka 40 ya ushirikiano.

Aliwataka walengwa kutumia vizuri fedha wanazozipata ili ziwasaidie wao na familia zao.

Alisema kupitia TASAF wataendelea kushirikiana na Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema serikali ya Uswisi ilitoa dola milioni 16.4 kwa ajili ya kusaidia mpango huo.

Pia alisema Uswisi wako tayari kuendelea kusaidia TASAF, ili kuhakikisha wananchi wanyonge wanaendesha maisha yao.

Alisema sasa TASAF ipo katika programu ya awamu ya tatu kipindi cha pili ambapo kaya milioni 1.5 sawa na watu milioni tano wanufaika.

Kadhalika, alisema kaya zaidi ya 200,000 maisha yao yamebadilika kwani wameondoka katika umaskini sasa wana hali nzuri.

Alisema wanafunzi 872, ambao ni wanufaika wa mpango huo walifaulu na kwenda vyuo vikuu na kupata mikopo, hali inayoonyesha ufanisi mkubwa wa mpango kwenye jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Dk. Semistatus Mashimba, alisema Kijiji cha Wilunze kina walengwa 193 ambapo hadi sasa jumla ya Sh. milioni 44.8 zimelipwa kwa walengwa na Sh. 300,000 hazikuchukuliwa na walengwa kutokana na sababu mbalimbali kama vile kifo, kuhama na kutojitokeza.

Alisema mpango huo pia una programu za ajira za muda kama kilimo na ukarabati wa miundombinu ya barabara.

Mbunge wa Chamwino, Deogratius Ndejembi, alisema mpango huo umesaidia sana wananchi wa kaya maskini kwa ajili ya kuinua maisha yao na sasa wana uhakika wa kupata milo mitatu kwa siku.

Hata hivyo, alisema wanufaika wengi wamekuwa ni wafugaji wa kuku, bata na mbuzi, hivyo kujiongezea kipato pale wanapouza mifugo yao.





# PM aagiza huduma muhimu eneo la ujenzi Chuo cha VETA

**Na Grace Mwakalinga,**
CHUNYA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameuagiza uongozi wa Mkoa wa Mbeya, kuhakikisha huduma zote muhimu za kijamii zinapatikana katika Kijiji cha Mbugani eneo ambalo linajengwa Chuo cha Mamlaka ya Ufundi (VETA).

Majaliwa alitoa agizo hilo alipotembelea na kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa chuo hicho Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, huku akisisitiza ujenzi huo ukamilike kwa wakati ili wananchi wanapate elimu ya ufundi na kutimiza ndoto zao.

Alisema serikali imeamua kujenga vyuo vya ufundi maeneo mbalimbali nchini ili kufungua milango ya ajira kwa sababu mafunzo yanatolewa yanawezesha vijana kuajiriwa kwenye sekta mbalimbali.

"Serikali yenu ni sikivu tunaendelea kufanya mambo makubwa tunaimani vikwazo vingi tutavitatua, sasa ujenzi wa vyuo vya ufundi vitasaidia vijana waliokatisha ndoto zao, kurudi shule na kupata elimu itayowasaidia kupambana na umaskini," alisema Majaliwa.

Aliwashauri vijana nchini kutumia fursa hiyo vizuri kwa kuhakikisha wanasoma kwa bidii na kuzingatia maarifa wanayopewa ili watakapoajiriwa wakafanye kazi kwa ufanisi na maarifa makubwa.

Aidha, aliwasihi wananchi kuendelea kuyalinda maeneo yao ili kuepuka migogoro mbalimbali ikiwamo ya ardhi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alimwahidi Waziri Mkuu kusimamia kikamilifu ujenzi wa chuo hicho, ambacho kitakuwa msaada kwa wakazi wa Wilaya ya Chunya ambapo mbali na kuwapatia elimu lakini kitafungua fursa mbalimbali za ajira kwa mama ntilie na watu wengine.

Homera aliwaomba wataalamu wanaosimamia ujenzi huo kuongeza spidi na kuhakikisha thamani ya fedha itakayotumika iendane na hali halisi ya ujenzi wa chuo hicho.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (kulia), akikabidhi kompyuta kwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Shanes Nungu, kwa ajili ya kuongeza ufanisi na kurahisisha kazi katika Ofisi za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Mbeya wafurahia fursa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKAZI wa Jiji la Mbeya, wameishukuru serikali kwa kuamua maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Dunia, kitaifa kufanyikia jijini humo kwa maelezo kuwa imekuwa fursa kwao kujiingizia kipato.

Mmoja wa wakazi hao, Atupakisye Mwakyusa, alisema maadhimisho hayo yamekuwa fursa kwake kwa sababu amepata faida kubwa kupitia biashara yake ya nguo.

Alisema kwa sasa Jiji limekuwa na watu wengi hivyo mzigo anaouweka sokoni kila siku unakwisha.

Moses Abraham mfanyabiashara wa viazi soko la Sido alisema amekuwa akipokea wateja wengi na kwamba kwa kipindi cha wiki moja ametengeneza faida kubwa hivyo anajipanga kuongeza mzigo wa biashara yake.

"Tunamshukuru Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kuamua maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kitaifa yafanyike hapa jijini Mbeya, vipato vyetu vimeongezeka kupitia biashara hizi kwa sababu tunapokea wateja wa aina mbalimbali kwa kweli mji umechangamka," alisema Abraham.

Mbotolwe Mwaifwani ambaye ni mama ntilie eneo la CCM, alisema amekuwa akipokea wateja wengi kwenye mgahawa wake, na kwamba uhitaji umekuwa mkubwa kuliko biashara yake hivyo kupitia maadhimisho hayo ametengeneza faida na anakwenda kuongeza mtaji ili biashara yake ikue zaidi.

Nao baadhi ya wamiliki wa nyumba za wageni jijini humo, walisema kwa sasa kila eneo vyumba vimejaa kutokana na wingi wa wageni wanaoshiriki maadhimisho hayo.

# Waziri Jenista azitaka taasisi kushirikiana

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amezitaka taasisi zote zilizo chini ya wizara yake kufanya kazi kwa kushirikiana sambamba na kukosoana kwa hekima ili kuongeza ufanisi katika kazi.

Jenista alitoa kauli hiyo jana wakati wa kikao cha kukabidhi vitendea kazi zaidi ya kompyuta 10 vilivyotolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kuisaidia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) kutekeleza majukumu yake kilichofanyika jijini Mbeya.

Alisema taasisi zake zinapaswa kufanya kazi kwa kushirikiana na kuweka utaratibu wa kila idara kukosoa ili kuboresha utendaji kazi na wananchi kupatiwa huduma bora.

"Wizara yetu inasimamia sera na kutekeleza sheria mbalimbali zilizoanzishwa kwa mujibu wa katiba, tunapoadhimisha miaka 60 ya uhuru lazima tujipime tumefanya mambo gani na wapi turekebishe wizara hii ni nyeti lazima tufanye kazi kwa kushirikiana na kutatua vikwazo vinavyojitokeza kwa pamoja," alisema Jenista.

Aidha, alisema wizara hiyo mwaka 2022 itaanza kutoa tuzo kwa wafanyakazi bora kutoka taasisi mbalimbali zinazounda wizara hiyo kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na ari ya kufanya kazi.

Alisema kila taasisi itatoa mfanyakazi bora ambayo kwa mujibu wa mchakato atapatikana na kupatiwa zawadi kama motisha ya kufanya kazi kwa bidii.

Mkurugenzi Mtendaji wa WCF, Dk. John Mduma, alisema kompyuta walizozitoa ni sehemu ya kuonyesha ushirikiano miongoni mwa taasisi hizo katika kurahisisha utendaji kazi.

Alisema wataendelea kutoa vitendea kazi vingine katika taasisi nyingine zinazounda wizara hiyo ili kukabiliana na vikwazo na kutimizi majukumu yao ya kuwahudumia Watanzania.

Akipokea zawadi ya kompyuta kutoka kwa waziri huyo ambazo zilitolewa na WCF, Mkurugenzi Mkuu wa CMA, Shanes Nungu, alisema zitasaidia kushughulikia majalada na kesi mbalimbali kwa wakati.

Alisema tume yake imekuwa ikijitahidi kushughulikia kesi mbalimbali, na kwamba ili kufanikisha hayo kila mwaka wamejiwekea malengo ya kuyafikia ili kumaliza kesi na usuluhishi baina ya wafanyakazi na wadau wengine.

Alisema wameshughulikia kesi 160, lengo lao ni kushughulikia kesi nyingi zaidi, na kwamba kompyuta 55 walizonazo sasa zitachangia kurahisisha utendaji kazi.





# Hemed: Viwanda vitaitangaza Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI imesema uwapo wa viwanda vingi nchini vinavyozalisha bidhaa bora kutasaidia kuitangaza Zanzibar katika soko la kimaitafa.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alieleza hayo jana alipotembelea kiwanda cha Basra Textile Mills Limited kinachozalisha bidhaa za vitenge na kanga kilichoko Chumbuni Zanzibar.

Hemed alifurahishwa na hatua ya maendeleo ya kiwanda hicho katika uzalishaji wa bidhaa hizo jambo ambalo linaipelekea serikali kuwa na imani zaidi na uendeshaji, wa kiwanda hicho ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya mpango wa kukuza sekta ya viwanda nchini.

Aidha, aliwataka wamiliki wa kiwanda hicho kuwa wabunifu ili kuongeza kasi ya ushindani sambamba na kuongeza uzalishaji zaidi kwa maendeleo ya kiwanda hicho.

Hemed alisema ni jambo la faraja kuona bidhaa zinazozalishwa katika kiwanda zina kiwango bora na zinauzika katika soko la ukanda wa Afrika Mashariki, hatua ambayo inaendana na kasi ya serikali.

Hemed alimtaka meneja rasilimali watu katika kiwanda hicho kuhakikisha kuwa haki za wafanyakazi zinapatikana bila ya ubaguzi, likiwamo suala la maslahi pamoja na kupata mapumziko kwa mujibu wa kanuni za kamisheni ya kazi.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Pili wa Rais alimwagiza kamishna wa kazi kuhakikisha kuwa anayafuatilia malalamiko ya wafanyakazi wa kiwanda hicho na kuyapatia ufumbuzi kwa haraka ili kukuza uzalishaji na kuleta mafanikio kwa kiwanda hicho na serikali kwa ujumla.

Hemed aliwataka wafanyakazi wa kiwanda hicho kuwajibika kwa kufuata taratibu, sheria, kanuni na kufanyakazi kwa bidii ili kiwanda hicho kiendelee kuzalisha kama ilivyokusudiwa. Naye Meneja wa kiwanda hicho, Saleh Suleiman, alisema kiwanda kinazalisha bidhaa nzuri zenye ubora ndani ya nchi za Afrika Mashariki, pamoja na soko la uhakika katika ukanda huo, hali ambayo inapelekea hamasa zaidi kwa uzalishaji.

Alisema kwamba, licha ya mafanikio hayo, bado wanakabiliwa na changamoto ya gharama kubwa ya kusafirisha makaa ya mawe kutoka Songea hadi Zanzibar.

Akielezea hali ya ajira Kamishna wa Kazi Zanzibar, Fatma Iddi, alisema ni jambo la kuridhisha kuona asilimia 80 ya wafanyakazi katika kiwanda hicho ni Wazanzibari, jambo ambalo limesaidia kufikia shabaha ya serikali kupitia ilani ya CCM ya kutoa ajira 300,000.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wa kiwanda hicho, Said Hamza Muhamed, alisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kutokuwa na mapumziko, ukosefu wa mikataba kwa baadhi ya wafanyakazi pamoja kupewa barua za onyo mara kwa mara bila sababu za msingi.

## DC sasa aonyesha fursa kwa wavuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, Suzan Peter Kunambi, amewataka wavuvi kujiunga katika vikundi ili kufanya kazi zao kwa ushirikiano na ni rahisi kupata fursa zinazotolewa na serikali ikiwamo mikopo.

Aliyasema hayo jana Mtoni Kigomeni alipokuwa akizungumza na wavuvi wa eneo hilo, kwa lengo la kuwahamasisha kuanzisha vikundi vya ushirika.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeandaa programu maalum ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na wavuvi ni moja kati ya kundi litakalonufaika na mpango huo hivyo ni vyema kuwa tayari kwa kufuata masharti na watakaonufaika na fursa hiyo ni wale watakaokuwa wamesajiliwa.

Alisema kuwa mikopo hiyo haitakuwa na riba wala masharti magumu bali itatolewa kupitia Shirika la Fedha Duniani (IMF) zilizotolewa kwa ajili ya kupambana na UVIKO-19.

Mkuu huyo wa Wilaya alizitaja fursa zinazotarajiwa kutolewa na serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Bluu ni kuwapatia wavuvi boti zenye mashine na zana zote za uvuvi na mafunzo maalum ya teknolojia bora ya uvuvi.

"Dhamira ya serikali ni kuleta mageuzi makubwa katika shughuli zote zinazofanywa na wavuvi wa maji madogo. Lakini katika eneo la bahari kuu ili kupata maendeleo ya haraka na kuimarisha uchumi wa bluu nchini," alisema.

Wakieleza changamoto zao, wavuvi hao, walisema miundombinu katika eneo hilo wanaloitumia kwa ajili ya shughuli za uvuvi hairidhishi pamoja na kukosekana kwa huduma ya majisafi na salama na huduma za vyoo katika eneo ni changamoto inayowasababishia usumbufu katika shughuli zao.



Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'A', Unguja, Suzan Peter Kunambi (kulia), akizungumza na wavuvi wa mwalo wa Mtoni, wilayani humo jana.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mfumo malipo kimtandao rasmi mwezi huu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MFUMO wa ukusanyaji malipo kwa njia ya mtandao 'Zan Malipo' unatarajiwa kuanza rasmi Desemba mwaka huu katika taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, alisema lengo kuu la kuanza kwa mfumo huo ni kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali, ambapo zamani yalikuwa yakipotea kutokana na ukusanyaji wa kutumia vitabu vya risiti.

Waziri Jamal aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar wakati akifungua mafunzo kwa maofisa wa mifumo ya kidigitali na wahasibu wa taasisi za Serikali ya Zanzibar.

Alisema wazo la mfumo huo baada ya kufanyika kwa utafiti yakinifu juu ya mfumo uliopo wa kukusanya mapato kwa kutumia risiti, kitendo ambacho serikali ilikua inakosa mapato kwa njia mbalimbali.

Alisema kuna baadhi ya wananchi na wakusanyaji wa mapato walikuwa wanatumia risiti feki na noti bandia, mambo ambayo yalikuwa yakiikosesha serikali mapato.

Alisema pia mfumo huo ulikuwa unatumia harama nyingi za serikali kwa kuchapisha vitabu vya risiti ambavyo hutumika kwa kazi hiyo.

"Kabla ya kuanza kwa mfumo huu tulifanya utafiti wa kina na kubaini kwamba kuna haja ya kubadilika katika mifumo, ndio maana tukachukua hatua za haraka za kulibadilisha hili," alisema.

Kassim alisema mfumo huo pia utaiwezesha serikali kujua kila siku kiasi gani cha fedha zimekusanywa katika taasisi zake, lakini itawarahisishia wahasibu kupanga vyema rekodi zao za kimapato kwa kila siku.

"Lakini mfumo huo utaongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato katika taasisi zetu za serikali, lakini utaondosha usumbufu kwa wananchi wa kufuata huduma ya malipo maeneo ya mbali," alisema.

Alisema wakati umefika sasa kwa wananchi kuongeza kasi ya kufanya malipo ya serikali bila ya usumbufu, huku akisisitiza haja ya wasimamizi wa mfumo kuendelea kuwa waadilifu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Said Seif, alisema pamoja na mafunzo hayo, tayari taasisi zote za serikali zimeshaunganishwa katika mfumo huo, ambapo kuanzia Desemba mbili zitakua katika mfumo wa ukusanyaji kwa njia ya mtandao.

Alisema matarajio ya serikali kwamba mfumo huo utakuwa na mageuzi makubwa ya kiuchumi katika ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Basil Baligumiya, alisema kufanyika kwa mafunzo hayo anaamini kwamba suala la ukusanyaji wa mapato katika taasisi za Serikali ya Zanzibar litaimarika zaidi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SARAPHINA JOHN KIBESA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **P0359.0587** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule/kituo cha KIGURUNYEMBE CENTRE mwaka 2018, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Polisi taarifa **DOD/DOD/RB/118890/2019**

116594602

---

FORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 127 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late SEPERATUS HILBERT KAGASHANI - DECEASED**

**and**

**In the Matter of Application for letters of administration by ERICA SEPERATUS KAGASHANI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 21ST day of December, 2021.

**Dated at DAR ES SALAAM this 25th day of November, 2021.**

Registrar/Senior Resident Magistrate

116594302

---

Notice of date of hearing to appellant and respondent

**IN THE DISTRICT COURT OF MOMBA DISTRICT**
**AT CHAPWA**

**CIVIL APPEAL NO. .........16......OF 2021**

**Original Civil case no...129.........of ...2021...of the Tunduma primary Court of Momba at Chapwa.**

**...HAPPNESS MRAMBA................................APPELLANT**
**VERSUS**
**...MASUNGA MASEMBA ........................RESPONDENT**

**TO...MASUNGA MASEMBA ............ OF KAMSAMBA**

**TAKE NOTICE THAT;** The above mentioned Appeal has been fixed for mention /on ...2......the day of DECEMBER............2021 and you are required to enter appearance at such time and date.And you must file your reply within 14 days of service of this notice upon you.

**AND TAKE FURTHER NOTICE THAT,** if you default to enter appearance as aforesaid in the appeal and be determined in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this ...11......day of ...NOVEMBER 2021.........

RESIDENT MAGISTRATE
MOMBA

**RECEIVED A COPY OF NOTICE**
**DATE.......................**
**SIGNATURE**

116594502

---

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATIONH CAUSE NO 173 OF 2021**

**In the matter of the estate of the late PAULINA JANUARY BENEDICT and in the matter of application for letter of administration by MARY BENEDICTUS MUSHI**

**GENERAL CITATION**
**(rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letters of administration) is made to the above named petitioner

Objections to the should be filed on or before the 20th day of December 2021

**Dated at DAR ES SALAAM this 29th day of November 2021**

Registrar/Senior Resident Magistrate

116594202

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WEGESA MACHUMU ESSABA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **RANGE ROVER** yenye namba za usajili **T 791 BBE** chasisi namba **ASLLPAMM3WA395717** engine namba **42D42026702A,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/550400/2021**

116594702

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ARON MURIGA PETER**

Anatangaza kupotelewa na cheti Cha kidato Cha nne chenye index namba **S0333-0106** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWANZA SEKONDARI Mwaka 1996. Yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo Cha polisi. RB Namba. **MOR/MOR/RB/568241/2021**

116595102

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. ...... 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE VISCUS LAIMOS SICHONE**
**Of Mpunguzi within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY NEEMA JOHN MKONDYA and NESS VISCUS SICHONE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of PROBATE Rules Gn.369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 14/12/2021.
**Dated at Dodoma this 30/11/2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

1165895202

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF NYAMAGANA DISTRICT**
**AT MWANZA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 28 OF 2021.**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOSEPH DANIEL KATUGA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTER OF ADMINISTRATION BY LILIAN GERAZI BUYUYA**

**GENERAL CITATION**

Notice is hereby given that the above named petitioner has petition for grant of letter of Administration of the Estate of the above named deceased.
Any person with interest against the said Estate is called upon to file caveat if any, on or before 22nd December 2021 before granting the letter of Administration.
Dated at Mwanza this 30th November 2021

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
COURT OF DISTRICT DELEGATE- NYAMAGANA MWANZA

116595002

---

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa*

*Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Jeshi Uganda laishambulia ADF

**Kampala,** UGANDA

JESHI la Uganda, limeanzisha mashambulizi ya pamoja ya anga na ardhini dhidi ya kundi la waasi la Allied Democratic Forces (ADF), Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

**Takriban watu watano wameuawa katika milipuko hiyo ya mabomu.**

Msemaji wa Jeshi la Wananchi Uganda, Brigedia Jenerali Flavia Byekwaso, amethibitisha hayo kupitia akaunti yake rasmi ya twitter.

Alisema operesheni hizo zilifanywa na washirika wa Congo, dhidi ya kambi za ADF, hakutoa maelezo zaidi kuhusu maeneo ambayo mashambulizi hayo yamefanywa.

Mamlaka ya Uganda, inalaumu ADF, ambayo inashirikiana na Islamic State (IS) kwa msururu wa mashambulizi ya mabomu, tangu Oktoba.

Wiki mbili zilizopita, IS ilidai kuhusika na milipuko miwili ya mabomu nje kidogo ya Kituo Kikuu cha Polisi cha Kampala na karibu na bunge.

Takriban watu watano wameuawa katika milipuko hiyo ya mabomu, baadhi ya mashambulizi yakiwa ya kujitoa mhanga, kwa mujibu wa Polisi wa Uganda. **BBC**

## HRW: Taliban inaua, kuteka maofisa usalama

**New York,** MAREKANI

WAPIGANAJI wa kundi la Taliban wamewaua ama kuwapoteza zaidi ya maofisa 100 wa zamani wa polisi na ujasusi, tangu kundi hilo lichukuwe madaraka nchini Afghanistan, kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Haki za Binadamu la Human Rights Watch iliyotolewa, jana.

Shirika hilo limesema kwamba bado kumekuwa na kampeni ya kuwaandama maofisa wa zamani wa vyombo vya dola, waliohudumu kwenye serikali iliyopinduliwa, licha ya serikali ya Taliban kutangaza msamaha.

Ripoti hiyo ilibainisha kuwa vikosi vya Taliban vimekuwa vikiwasaka maofisa hao wa zamani, vikitumia rekodi za ajira za serikali na vimewalenga hata wale waliojisalimisha na kupokea barua za kuwahakikishia usalama wao.

Kwenye baadhi ya matukio, makamanda wa Taliban wamekuwa wakiorodhesha majina ya watu wa kuandamwa, wakidai kuwa walifanya makosa yasiyosameheka. **DW**

## Sura za waandishi wenye shaka kutambuliwa China

**Beijing,** CHINA

SERIKALI ya Jimbo la Henan, China limepanga kuweka mfumo wa kutambua sura za watu, ili kuwafuatilia waandishi wa habari wa kigeni, wanafunzi na watu wengine wanaotiliwa mashaka.

Kwa mujibu wa zabuni iliyotangazwa na jimbo hilo hivi jana, kamera 3,000 zitaunganishwa na vituo vya data vya jimbo na taifa.

Kamera hizo zitatuma ujumbe pale mtu anayeshukiwa anapojisajili hotelini, kununua tiketi ya ndege au kuvuuka mpaka wa jimbo hilo.

Mfumo huo utasimamiwa na maofisa 2,000 wa polisi, waandishi wa habari watagawanywa kwa mujibu wa rangi za taa za barabarani, yaani nyekundu, manjano na kijani - kwa mujibu wa haja ya kuwafuatilia.

Kwa mujibu wa zabuni hiyo, kamera hizo zitakuwa na nguvu ya kuitambua sura hata kwa mtu aliyevaa barakoa ama miwani ya giza. **DW**



Wahamiaji wakiwa wameweka kambi, huku polisi wa Ufaransa wakitoa taarifa ya kuvunja kambi ya makazi yao eneo la ufukwe wa karibu na Dunkirk, nchini humo jana. **PICHA: REUTERS**

## Chad yatoa msamaha kwa wapinzani 300

**N'djamena,** CHAD

JESHI la Chad, limetoa msamaha kwa waasi 300 pamoja na wapinzani, ikiwa ni hatua ya kutekeleza shinikizo kutoka kwa makundi ya upinzani, yaliyoalikwa kuhudhuria kikao cha pamoja cha kujadili hatima ya kisiasa ya taifa hilo lenye matatizo.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, msamaha huo ni kwa watu 296, waliokuwa wamezuiliwa kutokana tuhuma mbalimbali, zikiwano za kutoa maoni, ugaidi pamoja na kuhujumu serikali.

Makundi ya upinzani yalisema kwamba, msamaha huo ulikuwa mojawapo ya masharti kabla ya kuhudhuria kikao cha pamoja, kilichopendekezwa na Rais Mahamat Idriss Deby Itno, mwenye umri wa miaka 37, aliyechukua madaraka baada ya baba yake, Idriss Deby Itno, kuuawa wakati wa mapambano na wanamgambo, Aprili mwaka huu.

Wakazi wengi wa mji mkuu wa N'Djamena, wanasemekana kufurahishwa na msamaha huo wakiuelezea kama hatua ya kwanza kuelekea kuliunganisha taifa.

Kelma Manatouma, ambaye ni mtafiti wa masuala ya siasa kutoka Chuo Kikuu cha Nanterre karibu na Paris, ameiambia AFP kwamba hiyo ni hatua muhimu kuelekea maridhiano pamoja na kukubalika kwa uhalali wa utawala wa Deby. **VOA**

## China yaahidi dozi bilioni 1 Afrika

**Beijing,** CHINA

RAIS wa China, Xi Jinping, ameahidi kutuma barani Afrika dozi bilioni moja za chanjo ya Covid-19, ili kusaidia kuziba pengo la chanjo.

Rais alitoa ahadi hiyo wakati wa mkutano wa kilele wa China na Afrika. Kati ya bilioni moja, dozi milioni 600 zitatoka China moja kwa moja huku milioni 400, zitatoka kwa vyanzo vingine kama vile maeneo ya uzalishaji yatakayofadhiliwa.

China tayari imekuwa ikitoa dozi kwa nchi za Afrika. Ahadi ya hivi majuzi, inakuja huku kukiwa na kuenea kwa aina mpya ya virusi kwa jina Omicron, ambacho kiligunduliwa kwa mara ya kwanza Kusini mwa Afrika. **BBC**

# TEMBO WARRIORS MZIGONI ROBO FAINALI CANAF LEO

**Na Saada Akida**

BAO pekee la Timu ya Taifa ya Tanzania ya Wenye Ulemavu 'Tembo Warriors', lililofungwa na Frank Ngairo wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Sierra Leone kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, limetosha kuipeleka hatua ya robo fainali ya michuano Afrika (CANAF), ambayo hatua ya makundi ilikamilika jana.

Kutoka Kundi A ambalo zimo Tanzania na Sierra Leone, timu nyingine iliyotinga robo fainali ni Morocco ambayo nayo jana iliibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Uganda.

Tanzania itashuka tena dimba la Benjamin Mkapa leo kwenye mechi ya robo finali dhidi ya mshindi wa mechi ya jana jioni kutoka Kundi C kati ya Liberia na Cameroon.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Tanzania, Salvatory Edward, alisema anafurahi kuona wachezaji wake wamepambana kupata matokeo mazuri na kusonga mbele katika mashindano hayo.

Alisema wanasahau matokeo hayo na wanarudi uwanjani kufanyia kazi mapungufu yao ili kuendelea kufanya vizuri na kuhakikisha wanatumia mashindano hayo kama mifano kwa watu wenye ulemavu ambao wanafungiwa ndani.

"Licha ya kupambania taifa letu kwenda kushiriki Kombe la Dunia mwakani (nchini Uturuki), lakini tunahitaji kutumia fursa hii kuutangazia umma kwamba hata watu wenye ulemavu wanaweza kila sekta ikiwamo soka.

"Kuhusu mechi yetu ya kesho (leo), tumejipanga vizuri tuko tayari kukutana na timu yoyote iwe Liberia au Cameroon, kikubwa tumefanya maandalizi mazuri kuhakikisha tunakuwa miongoni mwa timu nne ambazo zitaenda kucheza Kombe la Dunia," alisema Salvatory.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Mchezo huo, Mosses Mabula, alisema wanaendelea vizuri na maandalizi kwa upande wa viongozi na wanaimani na timu hiyo kusonga mbele zaidi na kuiwakilisha vema Tanzania.

"Tunahitaji kutwaa ubingwa, kuheshimisha nchini kwa kuwa ni wenyeji pia tunahitaji kuwa miongoni mwa timu nne ambazo zitaenda kucheza Kombe la Dunia Uturuki mwakani," alisema Mabula. Timu nne zitakazotinga nusu fainali ya fainali hizo za Afrika zinazoendelea hapa nchini, zitakata tiketi moja kwa moja ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa Wenye Ulemavu mwakani nchini Uturuki.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata (kushoto), akipokea kombe kutoka kwa Shomar Kamna, ambaye ni nahodha wa timu yao ya mpira wa miguu, TRA SC, baada ya kuibuka washindi wa mashindano ya SHIMMUTA yaliyofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabingwa SHIMMUTA TRA SC waalikwa Uganda

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma na Kampuni Binafsi nchini (SHIMMUTA), Timu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA SC), wamepata mwaliko wa kwenda kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa na wenzao wa Uganda, imeelezwa jijini Dar es Salaam jana.

Mwaliko huo umetolewa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Uganda (URA), John Musinguzi, wakati akikipokea kikosi cha TRA SC kilichorejea Dar es Salaam kikitokea Morogoro katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka.

Kamishna Musinguzi aliwapongeza mabingwa hao na kuwataka waendeleze ushirikiano kazini na kwenye michezo wanayoshiriki.

Alisema anafahamu mafanikio katika michezo yatasaidia pia katika kuinua maendeleo ya nchi kupitia kazi za kila siku wanazozifanya.

"Ninaona hapa mbele kuna makombe matano, ninawaalika mje Uganda tucheze mechi ya kirafiki au wao watakuja huku (Tanzania), ninawaahidi pia kule Uganda tuna kikosi imara cha soka, sina uhakika katika michezo mingine, lakini tuanze kwanza na mpira wa miguu," alisema Musinguzi.

Naye Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, aliwapongeza wachezaji wake kwa kuendeleza ubabe katika mashindano hayo na kusema wameipa heshima kubwa taasisi hiyo.

Kidata aliwaambia ili kuhakikisha wanaendelea kufanya vizuri, ameshatenga 'fungu' la fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa uwanja wa michezo wanaotumia kufanya mazoezi.

Kiongozi huyo alielekeza kuwa, anataka kuona hadi kufikia Juni mwakani, marekebisho hayo ya uwanja yawe yamekamilika na tayari uanze kutumika.

"Nataka uwanja ufanyiwe marekebisho makubwa na uwe wa kisasa, hatuwezi kufanyia mazoezi katika viwanja vibovu halafu tukaenda kushindana katika viwanja vizuri, tutashindwa," Kidata alisema.

Msemaji wa timu hiyo, George Gassaya, aliushukuru uongozi wa TRA kwa kuwapa ushirikiano mzuri kuanzia wakati wa maandalizi hadi walipokuwa kwenye mashindano.

Gassaya alisema umakini na kujituma kwa wachezaji wa timu hiyo ndio sababu nyingine iliyowafanya kupata mafanikio na kuweza kutetea taji walilokuwa wanalishikilia la mashindano hayo.

"Tulipata muda mrefu wa mazoezi, unajua timu hii inaundwa na wachezaji kutoka mikoa yote ya Tanzania, na mpira si kazi yetu rasmi, ila tulipata muda mzuri wa kujiandaa na hatimaye tumeibuka mabingwa," alisema Gassaya.

TRA SC iliibuka Mabingwa wa SHIMMUTA mwaka huu baada ya kuwafunga wenzao kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCCA), bao 1-0.

## Morocco akalia kuti kavu Namungo

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, benchi lake la ufundi na Ofisa Mtendaji Mkuu, Omari Kaaya, wamekalia kuti kavu, baada ya uongozi kuwapa mechi moja tu ya Ligi Kuu, na kama watashindwa kupata matokeo mazuri, watatimuliwa.

Namungo inatarajia kucheza dhidi ya Ruvu Shooting Ijumaa ijayo kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Mmoja wa viongozi waandamizi wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, amesema kuwa baada ya kukaa na kutathmini mwenendo wa timu hiyo, wameamua kutoa mechi moja kwa benchi la ufundi na kama isipofanya vema basi wataachana nao.

"Kumekuwa na mgawanyiko kwenye timu, hakuna umoja kati ya benchi la ufundi wenyewe kwa wenyewe na viongozi pia, hivyo tumemwandikia pia Ofisa Mtendaji Mkuu kuhusu hilo.

Pia kuna malalamiko kuhusu Ofisa Mtendaji Mkuu wetu kwamba amekuwa akiwakataza watu ambao wametoka na timu hii tangu daraja la nne, kuonana na wachezaji kwa ajili ya kuwapa motisha. Hali hii imeleta mgawanyiko kwenye timu, inaonekana kabisa ndiyo sababu ya timu kutofanya vema, kwa hiyo sisi kama viongozi tumeamua kuchukua hatua kabla mambo hayajawa mabaya zaidi," alisema Zidadu, Mwenyekiti za zamani wa klabu hiyo.

Akilijibu hilo, Ofisa Mtendaji Mkuu amekana kuwa yeye siyo chanzo cha timu kufanya vibaya, badala yake jambo hilo wangeulizwa benchi la ufundi.

"Mimi kazi yangu kuangalia timu inasafiri vipi, inafikia wapi, wachezaji wako kwenye mazingira mazuri, kila mtu anapata stahiki yake, lakini kwenye uwanja mimi sihusiki zaidi ya benchi ya ufundi," alisema Kaaya.

Namungo inashika nafasi ya 13 mpaka sasa ikiwa na pointi sita, kwa mechi saba ilizocheza, ikishinda mechi moja tu, sare tatu na kupoteza tatu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MARTIAL AIVUTIA BARCA**
KLABU ya Barcelona inavutiwa na mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial, 25. **(Marca)**

**TORRES HUYOOO BARCA**
BARCELONA pia ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester City na Hispania, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 21. **(Mundo Deportivo)**

**POGBA AKUTANA NA PSG**
KIUNGO wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, hivi majuzi alizungumza na Rais wa Paris St-Germain, Nasser Al-Khelaifi lakini klabu hiyo ya Ufaransa inasisitiza kuwa hakukuwa na kitu zaidi ya kukutana tu. **(The Athletic)**

**PHILLIPS ATAKIWA LIVER**
KLABU ya West Ham inavutiwa na mlinzi wa kati wa Liverpool, Nathaniel Phillips mwenye umri wa miaka 24. **(Football Insider)**

**BARCA NA MKAKATI MZITO**
VIONGOZI wa Barcelona wamezungumza na wawakilishi wa Ferran Torres katika sherehe za Ballon d'Or ili kuhakikisha wanamsajili. **(Sport)**

**DIAZ AWANIWA LEEDS**
KLABU ya Leeds inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Real Madrid, Mariano Diaz mwenye umri wa miaka 28. **(Fichajes.net)**

**SARR AWINDWA INTER**
MALANG Sarr wa Chelsea mwenye umri wa miaka 22, analengwa na Inter Milan. Beki huyo wa Ufaransa amecheza mechi tatu pekee tangu ajiunge na Chelsea mwaka 2020. **(Sport Mediaset via Sun)**

**BRZOVIC AWANIWA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle ina mpango wa kutumia "kiasi kikubwa cha fedha" kumnasa kiungo wa kati wa Inter Milan, Marcelo Brozovic mwenye umri wa miaka 29. **(The Athletic)**

**MARI KUNG'OLEWA ARSENAL**
KLABU ya Flamengo inafikiria kumnunua mlinzi wa kati wa Arsenal na Hispania, Pablo Mari, Januari 28. **(Football London)**

**NUNO KUREJEA MZIGONI**
KOCHA Nuno Espirito Santo anataka kurejea haraka kwenye uongozi wa soka baada ya kufukuzwa Tottenham. **(Le 10 Sport)**



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AWEKA REKODI BALLON D'OR YA SABA

●●●Nilitaka kusema kwamba ni heshima kubwa kushindana na Robert [Lewandoski] aliyechukua nafasi ya pili...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi, ameibuka mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or kama mchezaji bora kwa mwaka 2021.

Messi aliisaidia nchi yake kushinda taji la Copa America, likiwa ndio taji lake la kwanza la kimataifa, na amefunga mabao 40 kwa mwaka 2021 kati ya hayo 28 akiifungia Barcelona, manne akiifungia PSG na nane akiifungia Argentina.

Mshambuliaji wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski ameshika nafasi ya pili, huku kiungo wa kati wa Chelsea na Italia, Jorginho akiwa wa tatu, wakati mshambuliaji wa Real Madrid na Ufaransa, Karim Benzema akishika nafasi ya nne.

Tuzo hiyo hupigiwa kura na waandishi 180 kutoka duniani kote, ingawa hakukuwa na taji lililotolewa mwaka 2020 kutokana na mlipuko wa jangwa la corona.

Messi na Cristiano Ronaldo walifanikiwa kushinda taji hilo mara tano kuanzia mwaka 2008, 2019 isipokuwa 2018 wakati kiungo wa kati wa Croatia, Luka Modric alipotawazwa kuwa mshindi.

Messi alikuwa tayari ameshaibuka mshindi mara nyingi zaidi ya mchezaji mwingine yeyote baada ya kushinda mwaka 2009, 2010, 2012, 2015 na 2019.

"Ni furaha isiyo kifani kuwa hapa tena," alisema katika sherehe hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa Theatre du Chatelet jijini Paris.

"Miaka miwili iliyopita nilidhani ndio mara ya mwisho. Watu walianza kuniuliza ni lini nitastaafu, lakini sasa niko hapa Paris nikiwa na furaha."

"Ni mwaka maalum kwangu na taji hili la Copa America, lilikuwa na maana kubwa kushinda 1-0 dhidi ya Brazil katika fainali iliyochezwa katika Uwanja wa Maracana na nilifurahia sana kusherehekea na raia wa Argentina.

"Sijui iwapo ndio tuzo bora katika maisha yangu, nimekuwa na kipindi kirefu cha mchezo, lakini ilikuwa tuzo muhimu pamoja na ile ya Argentina baada ya kupitia kipindi kigumu na changomoto chungu nzima na ukosoaji."

Messi pia alikuwa na maneno matamu kwa mshambuliaji wa Bayern Lewandoski aliyechukua nafasi ya pili.

"Nilitaka kusema kwamba ni heshima kubwa kushindana na Robert, alihitaji kushinda mwaka uliopita."

Kipa wa Paris St-Germain, Gianluigi Donnarumma, ambaye aliisaidia Italia kushinda Kombe la Euro 2020, alishinda tuzo ya kipa bora wakati kiungo wa kati wa Barcelona, Pedri mwenye umri wa miaka 19, alishinda tuzo mchezaji bora mwenye umri mdogo chini miaka 21.









# RANGNICK ATUA RASMI MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imemwajiri rasmi Ralf Rangnick kuwa kocha wa muda hadi mwishoni mwa msimu huu.

Raia huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 63, anamrithi mtangulizi wake, Ole Gunnar Solskjaer, ambaye alifutwa kazi Novemba 21, mwaka huu baada ya kufungwa mabao 4-1 na Watford.

Rangnick ameacha kazi yake kama mkuu wa michezo na maendeleo katika klabu ya Lokomotiv Moscow ili kuchukua mikoba hiyo.

"Ninafurahi kujiunga na Manchester United," alisema Rangnick akinukuliwa na BBC Sport.

Baada ya kukamilika kwa msimu huu, Rangnick atabakia hapo kwenye Uwanja wa Old Trafford kwa miaka miwili kama mshauri.

Mechi yake ya kwanza akisimamia Man United, ambao wako katika nafasi ya nane katika Ligi Kuu ya England huenda ikawa dhidi ya Arsenal kesho.

# Neymar kukaa nje wiki nane



**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imethibtisha kwamba, Neymar atakuwa nje ya dimba kwa wiki sita hadi nane baada ya kuumia kifundo cha mguu.

Nyota huyo wa Brazil alitolewa nje kwa machela katika mchezo wa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Saint-Etienne kwenye Ligi Kuu Ufaransa.

Kocha Mkuu wa PSG, Mauricio Pochettino, amesema hakutarajia majeraha hayo yangekuwa makubwa, lakini vipimo vimeonyesha Neymar kuwa ameumia vibaya kifundo cha mguu wa kushoto.

PSG ilisema katika taarifa yake Jumatano kuwa mchezaji huyo atakuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu na haikutarajia.

Kutokana na Neymar kuwa nje ya uwanja, inamaana kwamba atakosa mechi nane za mashindano, ukiwapo mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Club Brugge na pia dhidi ya Lyon Januari 8, mwakani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, amekuwa katika kiwango kisicho cha kuvutia msimu wa 2021-22, akifunga mabao matatu na kutoa asisti 14 kwenye mashindano yote.

## HABARI MICHEZO

5,865,580

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/12/21 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 02. 04/12/21 | 18:00 | Reading vs Hull City | 2.35 | 3.23 | 2.89 |
| 03. 04/12/21 | 18:00 | Bristol City vs Derby | 2.40 | 3.14 | 2.89 |
| 04. 04/12/21 | 18:00 | Barnsley vs Huddersfield | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 05. 04/12/21 | 18:00 | Newcastle vs Burnley | 2.24 | 3.31 | 3.21 |
| 06. 04/12/21 | 18:00 | Southampton vs Brighton | 2.42 | 3.30 | 2.90 |
| 07. 04/12/21 | 23:00 | Real Sociedad vs Real Madrid | 3.01 | 3.26 | 2.37 |
| 08. 05/12/21 | 14:30 | Bologna vs Fiorentina | 2.56 | 3.51 | 2.61 |
| 09. 05/12/21 | 16:00 | Rayo Vallecano vs Espanyol | 2.30 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/12/21 | 17:00 | Lorient vs Nantes | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 11. 05/12/21 | 17:30 | QPR vs Stoke City | 2.36 | 3.23 | 2.89 |
| 12. 05/12/21 | 19:30 | Aston Villa vs Leicester | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 13. 05/12/21 | 20:30 | Levante vs Osasuna | 2.45 | 3.20 | 2.95 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 01 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3327 | Algeria vs Sudan | 1.32 | 4.25 | 9.09 |
| 16:00 | 3067 | Niki Volou vs Panetolikos | 3.09 | 2.85 | 2.35 |
| 16:00 | 5063 | Egypt vs Lebanon | 1.48 | 3.61 | 6.74 |
| 17:30 | 3445 | CD Mensajero vs Zaragoza | 6.90 | 5.13 | 1.36 |
| 18:00 | 3750 | Levadiakos vs Olympiakos | 11.54 | 5.96 | 1.18 |
| 19:00 | 1499 | Simba vs Geita Gold FC | 1.28 | 4.85 | 8.92 |
| 20:00 | 1003 | Panathinaikos vs Volos | 1.52 | 3.74 | 5.76 |
| 20:30 | 2256 | Bologna vs Roma | 3.00 | 3.50 | 2.27 |
| 20:30 | 2345 | Inter vs Spezia | 1.18 | 7.22 | 13.04 |
| 20:30 | 4839 | Dinamo Zagreb vs HNK Rijeka | 1.64 | 3.43 | 5.02 |
| 21:00 | 1197 | Metz vs Montpellier | 2.57 | 3.31 | 2.67 |
| 21:00 | 1273 | SD Solares Medio Cudeyo vs Espanyol | 49.23 | 12.80 | 1.02 |
| 21:00 | 1779 | Cordoba vs Sevilla FC | 20.65 | 11.80 | 1.06 |
| 21:00 | 2805 | Angers vs Monaco | 3.19 | 3.24 | 2.26 |
| 21:00 | 3119 | Strasbourg vs Bordeaux | 1.70 | 3.88 | 4.57 |
| 21:00 | 3162 | SCR Altach vs Sturm Graz | 4.14 | 3.61 | 1.72 |
| 21:00 | 3711 | Brest vs St Etienne | 2.13 | 3.49 | 3.24 |
| 21:00 | 5116 | Troyes vs Lorient | 2.34 | 3.24 | 3.04 |
| 22:00 | 2553 | Saudi Arabia vs Jordan | 4.83 | 3.43 | 1.66 |
| 22:00 | 2705 | Feyenoord vs Heracles Almelo | 1.30 | 5.28 | 8.21 |
| 22:00 | 3976 | Sheffield Wed vs Hartlepool | 1.60 | 3.86 | 4.63 |
| 22:00 | 4175 | Sunderland vs Oldham | 1.30 | 4.84 | 8.14 |
| 22:00 | 4685 | UD Alzira vs Fuenlabrada | 5.35 | 3.96 | 1.57 |
| 22:00 | 5096 | Lommel United vs KAA Gent | 8.61 | 5.48 | 1.27 |
| 22:30 | 1805 | Kortrijk vs Oostende | 1.96 | 3.56 | 3.41 |
| 22:30 | 2107 | Queen of South vs Morton | 2.23 | 3.33 | 2.85 |
| 22:30 | 2172 | Southampton vs Leicester | 2.39 | 3.44 | 2.84 |
| 22:30 | 3492 | BSC Young Boys vs FC Lugano | 1.39 | 4.93 | 6.51 |
| 22:30 | 4505 | West Ham vs Brighton | 2.00 | 3.45 | 3.70 |
| 22:30 | 4837 | Wolverhampton vs Burnley | 1.94 | 3.40 | 4.00 |
| 22:30 | 5028 | Watford vs Chelsea | 9.77 | 5.38 | 1.30 |
| 22:30 | 5561 | AE Larissa vs PAOK | 8.30 | 4.73 | 1.30 |
| 22:30 | 5657 | Mechelen vs Cercle Brugge | 1.96 | 3.51 | 3.46 |
| 22:45 | 3256 | Racing Genk vs Brugge | 3.02 | 3.56 | 2.11 |
| 22:45 | 3484 | Sassuolo vs Napoli | 3.80 | 3.95 | 1.84 |
| 22:45 | 3525 | Genoa vs AC Milan | 5.19 | 4.09 | 1.61 |
| 22:45 | 4352 | St Mirren vs Ross County | 2.11 | 3.21 | 3.45 |
| 22:45 | 5375 | Aberdeen vs Livingston | 1.81 | 3.35 | 4.44 |
| 22:45 | 5507 | Dundee FC vs St Johnstone | 2.60 | 3.00 | 2.80 |
| 22:45 | 5915 | Hibernian vs Rangers | 6.31 | 4.34 | 1.46 |
| 23:00 | 1131 | Rennes vs Lille | 2.04 | 3.48 | 3.48 |
| 23:00 | 1572 | Lyon vs Reims | 1.48 | 4.58 | 5.78 |
| 23:00 | 1828 | CFI Alicante vs Betis | 39.48 | 17.76 | 1.01 |
| 23:00 | 2709 | Clermont Foot vs Lens | 2.74 | 3.44 | 2.44 |
| 23:00 | 4058 | Real Madrid vs Athletic Bilbao | 1.50 | 4.31 | 6.19 |
| 23:00 | 4339 | Paris St Germain vs Nice | 1.47 | 4.57 | 5.97 |
| 23:00 | 4749 | CF Panaderia Pulido vs Real Sociedad | 39.48 | 17.76 | 1.01 |
| 23:00 | 5461 | Nantes vs Marseille | 3.09 | 3.39 | 2.24 |
| 23:15 | 2530 | Everton vs Liverpool | 6.80 | 4.90 | 1.41 |
| 23:15 | 5713 | Aston Villa vs Manchester City | 7.24 | 4.83 | 1.40 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SPORTPESA YAIDHAMINI TIMU YA BUNGE

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KAMPUNI ya Michezo na Burudani ya SportPesa imetoa vifaa vya michezo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20 kwa timu ya Bunge ambayo inatarajia kushiriki mashindano ya mabunge ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki jijini Arusha.

Makabidhiano hayo yalifanyika jana katika ukumbi wa habari Ofisi za Bunge kabla ya kuanza rasmi mashindano hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa ambaye ni Mwenyekiti wa Bunge Sports Club, Tarimba Abbas, kwanza aliishukuru SportPesa kwa udhamini wao katika kufanikisha ushiriki wa timu hiyo katika mashindano hayo.

"Hii ni mara ya pili kwa SportPesa kutoa udhamini huo ambapo mwaka 2017 walifanya hivyo kwenye mashindano ya Bunge. Tunapenda kuwahakikishia mashabiki kuwa tunatarajia ushindi wa kishindo huku tukipeperusha vema bendera ya Bunge la Tanzania.

"Tulikaa kikao na viongozi wa timu na wamenihakikishia kwamba watafanya vizuri ili kuhakikisha wanarudi na ushindi," alisema.

SportPesa imedhamini kwa kutoa vifaa vya timu zote nane ikiwamo mipira ya miguu, kikapu, pete, vifaa vya dart, kuvuta kamba pamoja na michezo mingine zikiwamo sare za viongozi.

Kwa upande wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania, ambaye ni mwakilishi wa Katibu wa Bunge, Mohammed Mwanga, mbali na kuishukuru SportPesa kwa vifaa hivyo, aliwaomba wabunge kuvitendea haki.

"Nawatakia kila la kheri kwenye mashindano yatakayofanyika Karatu na Arusha, safari njema. Mcheze kwa ushikamano na kuhakikisha mnaondoka na ushindi.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa SportPesa, Sabrina Msuya, aliishukuru timu ya Bunge kwa kujitoa na kuunda timu mbalimbali na kuwatakia kila la kheri kwenye mashindano hayo yatakayohusisha nchi za Afrika Mashariki.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa ambaye ni Mwenyekiti wa Bunge Sports Club, Tarimba Abbas (watatu kutoka kulia mbele), akiwa na wabunge wanaounda timu ya Bunge na viongozi wao baada ya kukabidhi vifaa mbalimbali vya michezo kuelekea mashindano ya mabunge ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayofanyika jijini Arusha hivi karibuni. **PICHA: SPORTPESA**

# Aggrey Morris ajiweka sokoni

**Na Dennis Fussi**

MLINZI wa Azam FC, Aggrey Morris, amesema anatarajia kurejea uwanjani baada ya usajili wa dirisha dogo linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Morris ni miongoni mwa wachezaji watatu waliosimamishwa na klabu yao hivi karibuni kwa muda usiojulikana ikielezwa sababu ni utovu wa nidhamu akiwa pamoja na Mudathir Yahya na Abubakari Salum 'Sure boy'.

Akizungumza na gazeti hili kuhusu kurejea kwake uwanjani, Morris alisema anatarajia kurudi kwenye dirisha dogo ila hakutaka kusema ni klabu gani.

"Ninatarajia kurejea uwanjani dirisha dogo, siwezi kusema timu gani, bado nina mkataba na Azam FC na nina uheshimu," alisema.

Baada ya kusimamishwa, wachezaji hao walipeleka mashtaka kwenye Chama cha Haki za Wachezaji (Sputanza), kujua mustakabali wao ili kulinda vipaji vyao. Lakini taarifa ya Azam ilisema kwamba, wachezaji hao wameonyesha utovu wa nidhamu kwa meneja wa timu, wachezaji wenzao, benchi la ufundi na viongozi wa klabu kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

Awali, taarifa ya Azam FC, ilisema wachezaji hao walimfuata ofisini kwake Meneja wa klabu hiyo, Luckson Kakolaki, na kumtolea maneno yasiyo na staha Septemba 18, mwaka huu siku ya mchezo wa pili wa raundi ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Horseed FC ya Somalia.

# Michezo

Jumatano Desemba 1, 2021

Nipashe





**Messi aweka rekodi Ballon d'Or ya saba**

MNATUSOMA?....




Fiston Mayele (kushoto), akishangilia na Feisal Salum 'Fei Toto', aliyemmegea pasi ya mwisho kuifungia Yanga bao la pili kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya jana na timu hiyo kushinda mabao 2-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# YANGA BADO YA MOTO

## ●●●Mayele, Fei Toto wanoga tena Mbeya Kwanza ikilala, Nabi ageuka bubu mechi ya watani, aomba...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na wachezaji wawili wa kigeni, Mrundi Saido Ntibazonkiza na Mkongomani, Fiston Mayele ndani ya dakika 25 tu za mwanzo, jana na kuiwezesha timu ya Yanga kuzoa pointi tatu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, dhidi ya Mbeya Kwanza, yamedhihirishia kuwa bado ni wa moto baada ya mechi iliyopita kutoka sare.

Yanga ambayo mechi iliyopita ugenini dhidi ya Namungo FC ilitoka sare ya bao 1-1, jana ilimaliza biashara mapema na kupata ushindi wa mabao 2-0 uliowawezesha kufikisha jumla ya pointi 19 na mabao 12, ikifungwa mawili na kuzidi kujichimbia kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa Mbeya Kwanza kupoteza nyumbani tangu kuanza kwa Ligi Kuu na ya pili kwa ujumla kwao kupoteza msimu huu.

Dalili za Yanga kuondoka na ushindi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, zilionekana mapema tu tangu kuanza kwa mechi hiyo, kwani dakika ya pili, Fiston Mayele nusura auweke mpira ndani ya wavu alipounganisha kwa kichwa mpira wa faulo uliopigwa na Saido Ntibazonkiza, lakini mpira ulitoka mita chache kwenye lango la wapinzani wao.

Ntibazonkiza aliipatia Yanga bao la kwanza kwa mkwaju wa faulo dakika ya 17, uliotokana na Feisal Salum kuangushwa nje kidogo ya eneo la hatari, na mpigaji alipiga faulo ya moja kwa moja iliyotinga wavuni, kipa wa Mbeya Kwanza, Hamad Kadedi na walinzi wake wakiwa wamesimama.

Dakika tatu baadaye Deus Kaseke aliikosesha Yanga bao, alipopaisha mpira akiwa yeye na goli, baada ya kipa na mabeki wa Mbeya Kwanza kujichanganya wenyewe.

Nusura Hamisi Kanduru aipatie Mbeya Kwanza bao dakika ya 22, alipopiga mpira wa adhabu ndogo na kumpiga kipa Djigui Diarra, lakini uligonga mwamba wa juu na kurejea uwanjani.

Zilipita dakika tatu baada ya wenyeji kukosa bao, ndipo Yanga ilipoandika bao la pili, likifungwa na Mayele, kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Fei Toto, lakini ni Mayele mwenyewe ndiye alianzisha shambulizi hilo kwa kumpa mtoa pasi ya mwisho na yeye akaingia ndani kusubiri krosi fupi, kabla ya kuijaza nyavuni.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, Yanga ikiwatoa wafungaji wa mabao, Mayele na Ntibazonkiza, Zawadi Mauya, na Kaseke, wakiwaingiza Yusuph Athumani, Kibwana Shomari, Hetier Makambo na Farid Mussa wakati Mbeya Kwanza iliwatoa Kanduru na Doglas Ambakisye, na kuwaingiza Paul Peter na Jimmy Shoji.

Ni mabadiliko ambayo yaliwasaidia Mbeya Kwanza, kwani ilitawala karibuni kipindi chote cha pili, lakini wachezaji wao hawakuwa makini wanapofika eneo la mwisho la lango la Yanga.

Pamoja na kufanya mashmbulizi mengi, shambulio la hatari zaidi lilikuwa ni dakika ya 77, wakati Chesco Masimba alipowazidi maarifa mabeki wa Yanga, Bakari Mwamnyeto na Dickson Job na kuupora mpira, lakini pasi yake haikuwa na muunganishaji, mpira ukatoka nje.

Mbeya Kwanza imebaki na pointi zake saba kwenye mechi saba ilizocheza, ikiwa kwenye nafasi ya 11, kabla ya mechi za jana na leo.

Baada ya mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alipoulizwa endapo ushindi huo ni dalili nzuri kuelekea mechi ya watani wa jadi, dhidi ya Simba Desemba 11, mwaka huu, aliomba subira kwanza kuzungumzia mchezo huo.

"Subirini kwanza swali hilo mtaniuliza baadaye, kwa sasa tunashukuru kupata ushindi tunaenda kujipanga kwa mechi hiyo," alisema.

## Simba, Yanga mlima mrefu FA

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Kombe la FA, Simba wataanza hatua ya 64 bora ikiwa ni raundi ya tatu ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini, maarufu FA Cup dhidi ya JKT Tanzania, huku watani zao wa jadi wakirudishwa tena kwa wapinzani wao wakubwa kwenye michuano hiyo, Ihefu FC kukumbushia mechi ya mwaka 2018.

Mechi hizo zinatarajiwa kuchezwa Desemba 14 na 15, huku siku moja ikiongezwa ya dharura endapo kutakuwa na mwingiliano wa ratiba ya Ligi Kuu, au kuchelewa kwa timu kufika kituoni ambayo ni Desemba 16, mwaka huu.

Kwa mujibu wa droo iliyofanyika jana mchana jijini Dar es Salaam, Simba ambayo ilitwaa kombe hilo kwa kuifunga Yanga bao 1-0 Julai 25, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma, itaaanza kutetea kombe lake dhidi ya maafande wa JKT Tanzania ambao walishuka daraja msimu uliomalizika na sasa wanacheza ngazi ya Championship.

Wanafainali wa msimu uliopita, Yanga, wao wameonekana kupewa mpinzani wao mkubwa kwenye michuano hiyo, Ihefu FC, kukumbushia mechi kali iliyofanyika Januari 30, 2018 kwenye Uwanja wa Sokoine, wakati huo ikiwa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Kwenye mechi hiyo, Yanga ilipata wakati mgumu ikionekana imeshalala, ikisawazisha bao dakika za majeruhi na kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-3. Baadaye Ihefu ilipanda Ligi Kuu msimu wa 2020/21, lakini ikateremka msimu huo uliomalizika na sasa ipo ngazi ya Championship.

Timu ya Azam FC yenyewe itakuwa na kibarua kizito itakapocheza na maafande wasiotabirika, Green Warriors.

Ratiba inaonyesha kuwa Dodoma Jiji itacheza dhidi ya Pan African, Biashara United dhidi ya Nyota Academy, Mtibwa Sugar dhidi ya Tunduma United, Mbeya City itakuwa mwenyeji wa African Sports, Namungo FC itaikaribisha timu korofi ya Mashujaa, huku Kagera Sugar ikiivaa TRA.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >